VOLUME IV

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA MBUNGE, JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

PARLIAMENT OF TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (2020—2025)

## TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

VOLUME IV

**JUNI 30, 2022**

**YALIYOMO**

1. YALIYOMO…………………………………...………… 1

2. UTANGULIZI…………………………………………….. 2

3. MIRADI YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) YA MWAKA 2020-2025
*(TAARIFA YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022)*

3.1 MIRADI YA ELIMU……………………………………. 5

3.2 MIRADI YA AFYA…………………………………….. 61

3.3 MIRADI YA KILIMO, UVUVI NA UFUGAJI………………. 77

3.4 MIRADI YA MAJI……………………………………..87

3.5 MIRADI YA UJENZI WA BARABARA…………………….. 95

3.6 MICHEZO NA UTAMADUNI…………………….............. 103

4. MENGINEYO…………………………………………. 107

5. HITIMISHO…………………………………………… 110

6. SHUKRANI……………………………………………. 112

**UTANGULIZI**

Kitabu hiki ni moja ya chapisho linalotoa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kuanzia Mwaka 2020 hadi 2025

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, ameweka utaratibu wa kuchapisha vitabu vinavyoelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani za Uchaguzi za CCM ndani ya Jimbo lao kama ifuatavyo:

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020:**

Vitabu viwili (2) vilichapishwa:

(i) Julai 7, 2019 (Volume I)

(ii) June 30, 2020 (Volume II)

**Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025:**

Machapisho ya utekelezaji wa Ilani hii ya Uchaguzi yameanza kutolewa kwenye vitabu kama ifuatavyo:

(iii) Juni 30, 2021 (Volume III)

(iv) Juni 30, 2022 (Volume IV)

Jimbo la Musoma Vijijini lina jumla ya Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374. Jimbo letu limechagua vipaumbele vitano kutoka ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025. Vipaumbele hivyo ni: (i) Elimu, (ii) Afya, (iii) Kilimo, Uvuvi na Ufugaji, (iv) Tabianchi na Mazingira, na (v) Michezo na Utamaduni.

Maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano, raslimali watu, na taasisi za fedha na uchumi ni nyenzo muhimu zinazohitajika kufanikisha utekelezaji wa miradi inayoibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano.

Wanavijiji kwa kushirikiana na viongozi wao wa ngazi mbalimbali hupendekeza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji yao, na huchangia nguvukazi na mali zao kwenye utekelezaji wa miradi ya chaguo lao. Uanzishwaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya

wanavijiji unafuata taratibu na sheria zilizowekwa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi wa Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan inapongezwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kwa kuendelea kutoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea kuboresha na kuimarisha uchumi na ustawi wa wananchi wa Jimbo hili.

Kitabu hiki (Volume IV) ni chapisho linaloelezea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini kwa kipindi cha mwaka mmoja wa fedha (1 Julai 2021-30 Juni 2022). Vilevile, taarifa hii inaonesha michango mingi na mikubwa iliyotolewa na Serikali Kuu, Mbunge wa Jimbo, Wanavijiji, baadhi ya Wazaliwa wa Jimboni mwetu, na Wadau wengine wa maendeleo ya Musoma Vijijini.

Kitabu hiki, kama vilivyo vingine vyote vya taarifa za maendeleo ya Jimbo la Musoma Vijijini hugawiwa bure. Haviuzwi!

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ELIMU

**(30 Juni 2022 – 1 Julai 2021)**

**Tarehe 30 Juni 2022: Idadi ya shule Jimboni mwetu ni:**

*Shule Shikizi: 13 zinatumika na upanuzi wake unaendelea

*Shule za Msingi: 111 Serikali & 3 Binafsi

Maktaba 3 zimejengwa na zinatumika & 2 nyingine zinajengwa

*Shule za Sekondari: 22 Kata/Serikali, 2 Binafsi & 10 zinajengwa (Kata)

4 zina Maabara 3 (fizikia, kemia na bailojia)

18 zinaendelea kujenga Maabara hizo

## TAIFA LINAHITAJI WANASAYANSI WENGI NA MAHIRI – MUSOMA VIJIJINI KUANZA KUWA NA HIGH SCHOOLS ZA SAYANSI

Posted on April 20, 2022




*Tumepanga tuwe na High Schools angalau 5 za masomo ya sayansi ifikapo 2025.*

Jimbo la Musoma Vijijini linayo HIGH SCHOOL moja tu, nayo ni ya masomo ya ARTS (HKL, HGK na HGL). Hii ni Kasoma High School iliyoanza Mwaka 2014, na ni sehemu ya Sekondari ya Kasoma iliyofunguliwa Mwaka 1995.

Jimbo letu lina jumla ya:
*Sekondari 22 za Kata/Serikali
*Sekondari 2 za Binafsi (Madhehebu: Sabato & Katoliki)

Wananchi ndani ya Kata 21 za Jimbo letu wamepanga na wengine wameanza ujenzi wa Sekondari Mpya 10 – moja (Ifulifu Sekondari) ikiwa imepokea kutoka Serikalini Tsh MILIONI 470 za ujenzi wa Sekondari ya Kata hiyo itakayofunguliwa Juni 2022.

**UJENZI NA UBORESHAJI WA MAABARA**
WANAVIJIJI, kwa kushirikiana na SERIKALI yetu, wameamua kujenga na kuboresha MAABARA zote za Sekondari zetu. MAABARA hizo ni za masomo ya Fizikia, Kemia na Baiolojia.

Mbali ya kuboresha uelewa na ufundishaji wa masomo hayo kwa WANAFUNZI wa KIDATO cha I hadi IV, lengo jingine ni kuanzisha HIGH SCHOOLS za MASOMO ya SAYANSI (k.m., PCM & PCB) Jimboni mwetu.

Tumepanga tuwe na High Schools angalau 5 za masomo ya sayansi ifikapo 2025.

WANAVIJIJI wa Kata ya Kiriba yenye Vijiji 3 wameamua kujenga MIUNDOMBINU ya HIGH SCHOOL ya masomo ya SAYANSI.

SHUKRANI zinatolewa kwa:
*Serikali yetu chini ya uongozi wa Rais wetu, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan
*Benki za NBC, NMB, CRDB na TPB
*Baadhi ya Wazaliwa wa Kata ya Kiriba

Usisahau kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu:
www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KATA ISIYOKUWA NA SEKONDARI YAKE YAPOKEA SHILINGI MILIONI 470 KWA AJILI WA UJENZI WA SEKONDARI YA KATA HIYO

Posted on January 25, 2022



*Kikao cha Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, na VIONGOZI wa ujenzi wa Ifulifu Sekondari ya Kata ya Ifulifu. Kikao kilifanyika Kijijini Kabegi, kwenye eneo la ujenzi wa Sekondari ya Kata.*

Kata ya IFULIFU ya Jimbo la Musoma Vijijini ndiyo KATA PEKEE isiyokuwa na Sekondari yake.

Wanafunzi wa Sekondari wa Kata hii wanasoma Sekondari za Kata jirani za Nyakatende na Mugango.

Kata hii ina VIJIJI 3 vya Kabegi, Kiemba na Nyasaungu.

Kijiji cha Nyasaungu kiko mbali na vijiji vingine na wakazi wake wengi ni wafugaji. Taarifa za ujenzi wa Sekondari ya Kijiji hiki cha Wafugaji ilitolewa, Ijumaa, 22.1.2022 (www.musomavijijini.or.tz)

**UJENZI WA IFULIFU SEKONDARI**

*Vijiji vya Kabegi na Kiemba vilianza ujenzi wa Sekondari yao JUNI 2017

*MICHANGO ya ujenzi wa Sekondari hii inatolewa na:
(i) Wanavijiji – fedha taslimu na nguvukazi
(ii) Mbunge wa Jimbo – fedha zake binafsi
*MAJENGO yaliyokamilishwa kwa nguvu za WANAVIJIJI na MBUNGE wao:
(i) Vyumba viwili vya Madarasa
(ii) Msingi wa Jengo la Utawala umekamilika
(iii) Matofali 1,200 yametengenezwa

**FEDHA ZA UVIKO-19/IMF ZIMEPOKELEWA**
Kata ya IFULIFU inayojenga Sekondari yake ya Kata tokea JUNI 2017, imepokea kwa shukrani nyingi mno SHILINGI MILIONI 470 kutoka Serikali Kuu.

*Wanavijiji na Viongozi wa Kata ya Ifulifu wanatoa shukrani nyingi sana kwa Mhe Rais wao, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuimbuka Kata yao ambayo haina Sekondari yake, na ujenzi waliouanza unasuasua kwa ukosefu wa fedha. Fedha zimepatikana – KAZI IENDELEE!

Juzi, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, aliienda Kijijini Kabegi kufuatilia ujenzi wa Ifulifu Sekondari na kujadili na Viongozi wa Kata hiyo kuhusu matumizi bora ya TSH MILIONI 470 walizozipokea kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari ya Kata yao.

**USHAURI ULITOLEWA NA MBUNGE WA JIMBO**
*Vijiji 2 vya Kabegi na Kiemba vifanye VIKAO vya WANAVIJIJI kuwaeleza juu ya malengo ya fedha hizo (Tsh 470m) walizozipokea Katani
*Matumizi ya fedha hizo yawekwe wazi sana kwa wanavijiji
*Wanavijiji waendelee kuchangia nguvukazi ili miundombinu muhimu ya elimu ipatikane kutokana na fedha hizo.

*Ujenzi uende kwa kasi kubwa na kwa ubora unaokubalika
*Ifulifu Sekondari ifunguliwe Julai 2022 na Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza na kutoka Vijiji vya Kabegi na Kiemba waendelee na masomo yao kwenye Sekondari yao ya Kata.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## JAMII YA WAFUGAJI YAENDELEA KUJENGA SEKONDARI YAKE KIJIJINI MWAO

Posted on January 25, 2022



*Ziara ya Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo, Kijijini Nyasaungu, Kata ya Ifulifu. Mbunge wa Jimbo na Mwenyekiti wa Kamati ya ujenzi, Ndugu Joseph Chome (mwenye T-shirt ya rangi ya njano) wakiwa kwenye eneo la ujenzi wa Sekondari ya Kijiji cha Nyasaungu.*

Kijiji cha NYASAUNGU ni kimoja kati ya VIJIJI 3 vya Kata ya IFULIFU iliyo ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini. Ni hii Kata pekee isiyokuwa na Sekondari yake ndani ya Jimbo letu!

JIOGRAPHIA ya Kata hii imewalazimu WANAVIJIJI wa VIJIJI hivi vitatu kujenga SEKONDARI 2 kwa wakati mmoja.

Kijiji cha WAFUGAJI cha NYASAUNGU kimezungukwa na MITO na kiko mbali (kati ya kilomita 10 na 15) kutoka vijiji vingine viwili (Kabegi na Kiemba).

**N.B. Juzi, Ndugu Chacha alimueleza Mbunge wa Jimbo kwamba amelazimika kumpeleka mwanae akasome Sekondari ya Musoma Mjini baada ya mwanae kushindwa kwenda shuleni kwa siku 3 za mvua zilizonyeesha Kijijini mwao. Njia hazipitiki!**

Kwa hiyo, SEKONDARI 2 zinajengwa kwa mpangilio ufuatao:
*Nyasaungu Sekondari:
Inajengwa na Wanakijiji wa Nyasaungu (WAFUGAJI)

*Ifulifu Sekondari:
Inajengwa na Wanavijiji wa Kabegi na Kiemba. Taarifa zaidi za ujenzi wa Sekondari hii utatolewa baadae.

**UJENZI WA NYASAUNGU SEKONDARI**
Juzi, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo alitembelea Kijiji cha Nyasaungu kufuatilia ujenzi wa Sekondari ya Kijiji hicho ulioanza AGOSTI 2019.

Taarifa za ujenzi wa Sekondari hii ya WAFUGAJI wa Kijiji cha Nyasaungu imetolewa mara kadhaa.

**WACHANGIAJI WA UJENZI WAKE ni:**
*Wanakijiji wenyewe kwa vigezo vya wingi wa MIFUGO yao. Kwa mfano wenye ng’ombe zaidi ya 100 wanachangia Tsh LAKI 2 (200,000).
*Wanakijiji wanachangia NGUVUKAZI
*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo – fedha zake binafsi
*Mfuko wa Jimbo la Musoma Vijijini – fedha za Serikali.
Halmashauri yetu inaombwa nayo ianze kuchangia ujenzi huu.

**MIUNDOMBINU ILOYOKAMILISHWA:**
*Vyumba 3 vya Madarasa
*Choo chenye matundu sita (6)
*Jengo la Utawala: msingi umekamilishwa.

**MALENGO MAPYA YA NYASAUNGU SEKONDARI**
Wanakijiji wa Nyasaungu na Mbunge wao wamejiwekea MALENGO MAPYA ambayo ni:
*Jengo la Utawala likamilishwe kabla ya tarehe 30 Machi 2022
*Serikali iombwe kufungua Nyasaungu Sekondari JULAI 2022 iwapo miundombinu ya awali itakuwa imekamilika.

*SERIKALI ikisaidie Kijiji cha WAFUGAJI cha Nyasaungu kama ambavyo inasaidia JAMII ya WAFUGAJI sehemu nyingine za nchi yetu. Mbunge ameishawasilisha ombi hili kwa wahusika TAMISEMI.

**TUCHANGIE UJENZI WA NYASAUNGU SEKONDARI – Karibuni sana!**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# PROF MUHONGO ATEMBELEA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA

Posted on January 25, 2022



*Ugeni wa Prof Sospeter Muhongo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, kwenye Tegeruka Sekondari ya Kata ya Tegeruka.*

Jumatano, 19.1.2022, Prof Sospeter Muhongo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini alitembelea TEGERUKA SEKONDARI akifuatilia:

*Wanafunzi waliokwishafika shuleni hapo kuanza Masomo ya Kidato cha kwanza (2022)

Wanafunzi 54 kati ya 184 tayari wameanza masomo ya Kidato cha Kwanza. Leo ni siku ya tatu toka shule ifunguliwe.

Prof Muhongo amepiga PICHA na Wanafunzi hao wa Kidato cha Kwanza – baadhi ya Wazazi na Walimu wako kwenye picha hiyo hapo juu.

*Ujenzi wa Miundombinu kwenye Sekondari hiyo:

(i) Tegeruka Sekondari ilikuwa ya kwanza, ndani ya Jimbo letu, kukamilisha ujenzi wa VYUMBA VIPYA 3 vya MADARASA kwa kutumia fedha za UVIKO 19/IMF zilizopatikana kwa juhudi za Mhe Dkt Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. SHUKRANI NYINGI SANA kwa Mhe Rais wetu.

(ii) Sekondari haina MAABARA na MAKTABA. Mbunge wa Jimbo amekubali kutoa MICHANGO kwa kushirikiana na WANAVIJIJI wa KATA ya TEGERUKA kuanza mara moja ujenzi wa MAABARA 3 za masomo ya SAYANSI (Physics, Chemistry & Biology).

TEGERUKA SEKONDARI inahudumia VIJIJI 3 vya Kataryo, Mayani na Tegeruka. Ina jumla ya WANAFUNZI 509, na WALIMU 12, wakiwemo 5 wa Masomo ya Sayansi.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KIJIJI CHA PEMBEZONI CHA WAFUGAJI CHA NYASAUNGU KIMEAMUA KUJENGA SEKONDARI YAKE

Posted on December 13, 2021




*Wana-Nyasaungu wanapenda WATOTO wao 70 wa Kidato cha kwanza (2022) waanze masomo kwenye Sekondari yao waliyoanza kuijenga tokea Juni 2019.*

Kijiji cha NYASAUNGU ni moja ya Vijiji 3 (Kabegi, Kiemba & Nyasaungu) vya Kata ya IFULIFU. Hii ndiyo Kata pekee ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini ambayo haina Sekondari yake – ujenzi wa Sekondari 2 ulishaanza vijijini Kabegi (Ifulifu Sekondari) na Nyasaungu (Nyasaungu Sekondari)

Kijiji cha Nyasaungu kiko pembezoni na umbali kutoka vijiji vingine viwili vya Kata hiyo haupungui kilomita 10. Wakazi wake wengi ni WAFUGAJI.

WANAFUNZI wa Sekondari wa kutoka Kijiji hiki wanaenda kusoma Sekondari za Kata za jirani ambazo ni Mugango na Nyakatende. UMBALI wa kwenda na kurudi kwenye Sekondari hizo za Kata jirani ni takribani KILOMITA 20.

SERIKALI imetoa Tsh Milioni 470 kujenga Sekondari ya Kata ya IFULIFU ambayo itajengwa kwenye Kijiji cha KABEGI ambacho kiko takribani KILOMITA 10 kutoka Kijijini NYASAUNGU.

Kwa hiyo, Kijiji cha NYASAUNGU kinaendelea na ujenzi wa Sekondari yake ili kutatua TATIZO la UMBALI (na madhara yake) linalowakabili watoto wao.

UJENZI wa Sekondari ya Kijiji hicho ulianza JUNI 2019 na MICHANGO ya UJENZI inatoka kwa:

**Wanakijiji:**
Wanachangia nguvukazi na fedha taslimu (Tsh Milioni 19.7) kwa kuuza mifugo yao.

**Mbunge wa Jimbo:**
ameishachangia Mabati 108, Saruji Mifuko 30 na Nondo 20

**Mfuko wa Jimbo**:
umeishachangia Mabati 54 na Saruji Mifuko 80

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA NYASAUNGU**
*WANAKIJIJI/WAFUGAJI wanatuomba sana tuchangie sekondari yao.

*Wana-Nyasaungu wanapenda WATOTO wao 70 wa Kidato cha kwanza (2022) waanze masomo kwenye Sekondari yao waliyoanza kuijenga tokea Juni 2019.

**NB: Kijiji cha Nyasaungu – kimesimamisha ujenzi wa Zahanati ya Kijiji chao ili wakamilishe ujenzi wa Sekondari hiyo.**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI LAANZA UJENZI WA "HIGH SCHOOLS" ZA MASOMO YA SAYANSI

Posted on November 27, 2021



*Maabara za Kiriba Sekondari*

ELIMU: Jimbo la Musoma Vijijini (Kata 22 zenye Vijiji 68) lina idadi ifuatayo:

*Shule za Msingi za Serikali 111.
*Shule za Msingi za Binafsi 3
*Shule za Msingi mpya zinazojengwa (Shule Shikizi) 13
*Sekondari za Kata 22
*Sekondari za Binafsi 2
*Sekondari mpya zinazojengwa au zilizopangwa kujengwa 10
*High School 1 (iko Kasoma Sekondari) ya masomo ya "arts"

**MAABARA ZINAJENGWA KWENYE SEKONDARI ZOTE**

Sekondari zote 22 (na mpya zinazojengwa) zinajenga na kuboresha MAABARA 3 kwenye shule zao ambazo ni za Fizikia, Kemia na Biolojia.

Wananchi wa Kata ya Kiriba WAMEAMUA kuchangia ujenzi wa "HIGH SCHOOL" ya masomo ya SAYANSI (PCM & PCB) kwa kuanza ujenzi wa MIUNDOMBINU inayohitajika:

*Maabara 3 za Fizikia, Kemia na Biolojia: tayari zimekamilika na zinatumika.

*Jengo la Utawala limekamilika na linatumika.


*Ujenzi wa Mabweni umeanza, ambao utafuatiwa na ujenzi wa Bwalo la Chakula na Jiko.

**Unakaribishwa sana kuchangia ujenzi na uboreshaji wa MIUNDOMBINU ya ELIMU ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MUSOMA VIJIJINI IMEDHAMIRIA KUANZA KUWA NA "HIGH SCHOOLS" ZA MASOMO YA SAYANSI KUANZIA MWAKANI (Julai 2022)

Posted on August 23, 2021



*Wanafunzi na Walimu wakiwa kwenye MAABARA wakifanya "experiments" kwenye Maabara ya MUGANGO SEKONDARI.*

SEKONDARI zote 22 za KATA za Jimbo la Musoma Vijijini zina Miradi ya aina mbalimbali ya ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu ya kujifunzia na kufundishia.

MIRADI hiyo ni pamoja na ujenzi na uboreshaji wa MAABARA za masomo ya Sayansi (Physics, Chemistry & Biology).

MIRADI mingine ni ya ujenzi wa Vyumba vipya vya Madarasa, Maktaba, Mabweni, Vyoo na Nyumba za Walimu.

SHULE 2 za Sekondari za Binafsi, zinazomilikiwa na Kanisa Katoliki (RC) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA), nazo zinaboresha Miundombinu yake ya Elimu.

SEKONDARI mpya 10 zinazojengwa au zilizopangwa kujengwa zitakuwa na Miundombinu kama hiyo ya Elimu.

**UKAMILISHWAJI WA MAABARA 3 ZA MASOMO YA SAYANSI**

Baadhi ya Sekondari zetu tayari zimekamilisha na kuanza kutumia Maabara za Fizikia, Kemia na Biolojia.
SEKONDARI hizo ni:
*Kiriba
*Mugango
*Rusoli
*Bugwema (zinakamilika Sept 2021)

Kwa hiyo, MIPANGO ya ujenzi wa "HIGH SCHOOLS" za Masomo ya Sayansi utaanza kwenye SEKONDARI 4 zilizotajwa hapo juu kwa kuanza kujenga:
*Vyumba vipya vya Madarasa ya "High School"
*Bweni la Wanafunzi wa "High School"
*Bwalo la Chakula & Jiko lake

**MUHIMU:**

Michango ya awali kabisa inatolewa na WANANCHI WENYEWE ambao ni Wanavijiji na Viongozi wao, na Wazaliwa wa Vijiji vyenye MIRADI ya ujenzi – "KUJITOLEA"

**UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU YA MUGANGO SEKONDARI**

Ofisi ya Mbunge wa Jimbo imeishatoa taarifa za MAABARA 3 ya Sekondari za Kiriba na Rusoli. Leo inatoa taarifa za MAABARA za Mugango Sekondari

MKUU wa Mugango Sekondari, Mwl Chacha Ragita ameeleza yafuatayo:
*Sekondari ilifunguliwa Mwaka 1999
*Ina Wanafunzi 800
*Mahitaji ya Walimu ni 25, waliopo ni 18
*Mahitaji ya Vyumba vya Madarasa ni 20, vilivyopo ni 16
*Mahitaji ya Matundu ya Vyoo ni 34, yaliyopo 24
*Nyumba 18 za Walimu zinahitajika, zilizopo ni 4

MIUNDOMBINU iliyokamilika:
*Maabara za Fizikia, Kemia na Biolojia zote zipo zinatumika
*Maktaba ipo
*Matundu 2 ya Vyoo vya Walimu yapo.

MICHANGO ya Miradi ya ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu ya Sekondari hii inatolewa na:
*Serikali Kuu
*Wanavijiji
*Mbunge wa Jimbo
*Wadau wa Maendeleo

**WANAVIJIJI:**
na Viongozi wao wa Kata na Vijijini wanachangia fedha taslimu na NGUVUKAZI za kusomba mawe, mchanga, kokoto na maji ya ujenzi.

**SERIKALI KUU:**
imetoa michango mingi tokea Mwaka 1999, na hivi karibuni:
(i)TAMISEMI imetoa vifaa vyote vya Maabara zote tatu.
(ii)TAMISEMI imetoa Shilingi Milioni 75 kwa ajili ya ujenzi wa Bweni la Wasichana – ujenzi umeanza

MBUNGE wa JIMBO, Profesa Sospeter Muhongo amechangia:
(i)Saruji Mifuko 130
(ii)Vitabu zaidi ya 2,000 vya Maktaba

*MRADI wa MAJI (BADEA) umeunganisha Bomba la Maji kwenye Sekondari hii.

*SHIRIKA la Water Aid Tanzania limetoa Matenki 2 ya Maji yenye ujazo wa lita 5,000 kwa kila moja.

**UFAULU WA MITIHANI YA KIDATO CHA IV (2020)**
*Watahiniwa: 83
Div I – 4, Div II – 5, Div III-14, Div IV – 39 na Div 0 – 21

**MATOKEO YA KIDATO CHA II (2020)**
*Watahiniwa: 175
Div I – 8, Div II – 11, Div III-19, Div IV – 121 na Div 0-16

**OMBI: WADAU wa MAENDELEO tujitokeze kutoa MICHANGO ya ujenzi wa "HIGH SCHOOLS" za Masomo ya Sayansi Jimboni mwetu.**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## KATA ISIYOKUWA NA SEKONDARI YAKE YAAMUA KUJENGA SEKONDARI MBILI KWA WAKATI MMOJA

Posted on August 14, 2021



*Wananchi wa KIJIJI cha NYASAUNGU wakichimba Msingi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Jengo la Utawala la Nyasaungu Sekondari, Kata ya Ifulifu.*

KATA ya IFULIFU ni moja ya Kata 21 za Jimbo la Musoma Vijijini. Ni hii Kata pekee ambayo haina Shule yake ya Sekondari.

KATA hii inaundwa na Vijiji 3, ambavyo ni Kabegi, Kiemba na Nyasaungu.

Wanafunzi wa Sekondari wanaotoka kwenye Kata hii wanalazamika kutembea umbali mrefu kwenda masomoni kwenye Sekondari za Kata za jirani ambazo ni Kata ya Mugango (Mugango Sekondari) na Kata ya Nyakatende (Nyakatende Sekondari).

WANAVIJIJI wa Kata hii wameamua kujenga Sekondari Mbili (2) kwa utaratibu huu:
*Kijiji cha Nyasaungu, kinajenga Sekondari yake kwa kushirikiana na Mbunge wao wa Jimbo, Profesa Sospeter Muhongo
*Vijiji vya Kabegi na Kiemba, nao wanajenga Sekondari yao kwa kushirikiana na Mbunge wao wa Jimbo, Profesa Sospeter Muhongo

**NYASAUNGU SEKONDARI YA KIJIJI CHA NYASAUNGU**

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Nyasaungu, Ndugu Magesa Chacha ameeleza kuwa, ujenzi wa Sekondari yao ulianza JULAI 2019 na malengo yao ni NYASAUNGU SEKONDARI ifunguliwe mwakani (Januari 2022).

Mbali ya umbali mrefu wa kilomita 24 za watoto wao kutembea kwenda masomoni Mugango Sekondari, WANAFUNZI wa KIKE wanapambana na vishawishi vingi na baadhi kupata mimba na kukatisha masomo yao.

**MIUNDOMBINU INAYOJENGWA**

*Vyumba 2 vya Madarasa na Ofisi 1 tayari vimeishaezekwa
*Choo chenye Matundu 6, tayari kimeishaezekwa.
*Jengo la Utawala (msingi unachimbwa, na ujenzi utaanza hivi karibuni)
*Maabara 3 zitajengwa
*Maktaba itajengwa
*Nyumba za Walimu zitajengwa

**MAKUNDI YANAYOCHANGIA UJENZI WA NYASAUNGU SEKONDARI**

*Michango ya Kijiji cha Nyasaungu ni endelevu kulingana na mahitaji ya MIRADI ya MAENDELEO ya Kijiji hicho.

(i) Kaya zenye ng’ombe zaidi ya 100, michango yao ni Tshs 200,000 (Laki mbili)
(ii) Kaya zenye ng’ombe 99-50, michango yao ni Tshs 100,000 (Laki moja)
(iii) Kaya zenye ng’ombe chini ya 50, michango yao ni Tsh. 40,000 (elfu arobaini)
(iv) NGUVUKAZI za Wanakijiji za kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi.
(v) Michango ya MBUNGE wa JIMBO Profesa Sospeter Muhongo:
*Mabati 108
*Saruji Mifuko 35
*Nondo 20

**MFUKO wa JIMBO umechangia**
*Mabati 54
*Saruji Mifuko 80

WANAKIJIJI na VIONGOZI wao kwa kipekee kabisa, wanatoa shukrani nyingi sana kwa MBUNGE wao wa JIMBO, Mhe Prof Sospeter Muhongo kwa jitihada kubwa anazoziweka kwenye UTEKELEZAJI wa MIRADI ya MAENDELEO ya Kijiji chao – amechangia madawati na vitabu kwenye Shule yao ya Msingi. AMEFUFUA na kuchangia ujenzi wa Zahanati ya Kijiji chao.

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA NYASAUNGU**
WAZALIWA wa Kijiji cha Nyasaungu, na Kata nzima ya Ifulifu wanaombwa kutoa MICHANGO kwenye ujenzi wa Nyasaungu Sekondari ambayo itapokea Wanafunzi kutoka Kata yao na Kata za jirani.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# UJENZI NA UBORESHAJI WA MAABARA ZA MASOMO YA SAYANSI VYAHAMASISHA WANAFUNZI KUPENDA MASOMO HAYO

Posted on August 7, 2021



*Mkuu wa Shule & Diwani wakiwa ndani ya Maabara ya Biolojia*

**MALENGO YETU:**

(i) SEKONDARI zote 22 za Kata/Serikali za Jimbo la Musoma Vijijini ziko kwenye UJENZI & UBORESHAJI wa MAABARA 3 za Masomo ya FIZIKIA, KEMIA na BIOLOJIA.
Kazi hiyo imepangwa ikamilike kabla ya Disemba 2022.

(ii) SEKONDARI 2 za Binafsi (Kanisa Katoliki & SDA) nazo zimeshawishiwa kufanya hivyo

(iii) SEKONDARI 10 mpya zinazojengwa au zitakazoanza kujengwa hivi karibuni zitakuwa na MAABARA hizo 3 & MAKTABA

(iv) SEKONDARI zilizokamilisha ujenzi na uboreshaji wa MAABARA hizo 4 zianze matayarisho ya kuwa na “HIGH SCHOOLS” za Masomo ya SAYANSI

(v) KAMPENI maalumu zianzishwe za kushawishi na kuvutia WANAFUNZI kupenda kusoma MASOMO ya SAYANSI

**RUSOLI SEKONDARI**

Sekondari hii ni ya Kata ya Rusoli. Ilifunguliwa Mwaka 2010 kuhudumia Wanafunzi wa kutoka Vijiji 3 (Buanga, Kwikerege na Rusoli) vya Kata hii.

MKUU wa Sekondari ya Rusoli, Mwl Tausi Juma ameeleza yafuatayo kuhusu Shule hii:

(i) Ina Wanafunzi 444
(ii) Mahitaji ya Walimu ni 15, waliopo ni 13 na kati ya hao 6 ni wa Masomo ya Sayansi
(iii) Ina MAABARA 3 za Fizikia, Kemia na Biolojia
(iv) Mahitaji ya Vyumba vya Madarasa ni 12, vilivyopo ni 10

**UJENZI & UBORESHAJI WA MAABARA ZA RUSOLI SEKONDARI**

Ujenzi na uboreshaji wa MAABARA hizi unashirikisha:

*Serikali
*Wanavijiji (NGUVUKAZI)
*Wazaliwa wa Kata ya Rusoli
*Mbunge wa Jimbo

**MATUMIZI YA FEDHA ZA SERIKALI**

MKUU wa Rusoli Sekondari, Mwl. Tausi Juma ameeleza kuwa Serikali kupitia Mradi wake wa EP4R imetoa:

(i) SHILINGI MILIONI 30 kwa ajili ya:
*Ukamilishaji wa Maabara ya FIZIKIA na samani zake
*Ujenzi wa TENKI la kuvunia maji ya mvua ya kutumia kwenye Maabara
*Kukamilisha uwekaji wa mfumo wa gesi na umeme kwenye Maabara.

(ii) SHILINGI MILIONI 25 kwa ajili ya ukamilishaji wa Maabara ya KEMIA

(iii) VIFAA vya Maabara vilitolewa na TAMISEMI
*Inakadiriwa kwamba Asilimia 75 (75%) ya Wanafunzi wa Kidato cha I & II wa RUSOLI SEKONDARI wamehamasika na kuvutiwa sana na MASOMO ya SAYANSI ya VITENDO (practicals) kwenye MAABARA zao.

**MICHANGO MINGINE ILIYOKWISHATOLEWA RUSOLI SEKONDARI**

(i) WAZALIWA wa Kata ya Rusoli kupitia Kikundi chao kiitwacho, "YEBHE CHIKOMESHE" kimetoa MICHANGO MINGI kwenye Sekondari hii ikiwemo ya VIFAA vya MAABARA, COMPUTER, PRINTER & PHOTOCOPY

Kikundi hiki kinaongozwa kwa umahiri mkubwa na Ndugu JEFF MAKONGO.

Vilevile, "Yebhe Chikomeshe" kimejenga NYUMBA (two in one) ya WALIMU wa Sekondari hii.

Kimechimba KISIMA cha MAJI kwa matumzi ya Kijiji cha Rusoli – AHSANTE SANA SANA "YEBHE CHIKOMESHE" – Kikundi cha Maendeleo yanayoonekana!

(ii) MBUNGE wa JIMBO, Profesa Sospeter Muhongo amechangia:

*Saruji Mifuko 70
*Posho ya Mwalimu wa Kujitolea wa Masomo ya Sayansi
*Vitabu zaidi ya 2,000 vya Maktaba

DIWANI wa Kata ya Rusoli, Mhe Boaz Nyeura na Viongozi wengine wa Kata na Vijiji wanaendelea kutoa SHUKRANI NYINGI SANA kwa MICHANGO & MISAADA wanayopokea kutoka SERIKALINI na kutoka kwa WADAU wengine wa MAENDELEO ya Kata yao, hasa kutoka kwa Mbunge wao wa Jimbo, na Kikundi cha, "Yebhe Chikomeshe."

**UFAULU WA MITIHANI WA RUSOLI SEKONDARI**


*MATOKEO YA KIDATO CHA II (2020)
Watahiniwa: 107
Div I= 6, Div II= 9, Div III=26 na Div IV =66

***MATOKEO YA KIDATO CHA IV (2020)**
Watahiniwa: 64
Div I= 1, Div II= 6, Div III= 7, Div IV= 44 na Div 0= 6

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SEKONDARI YA ISHIRINI NA MBILI (22) YAFUNGULIWA MUSOMA VIJIJINI

Posted on July 25, 2021



*WANAFUNZI wa KIDATO cha KWANZA wa Seka Sekondari wakijisomea Madarasani mwao, SEKA SEKONDARI ambayo ni MPYA na imefunguliwa tarehe 5.7.2021. Hii ni Sekondari ya pili ya Kata ya Nyamrandirira*.

JIMBO la Musoma Vijijini lenye Kata 21, Vijiji 68 na Vitongoji 374, linaendelea na utaratibu wake wa kutatua MATATIZO ya MIRUNDIKANO ya Wanafunzi madarasani kwenye Shule za Msingi na Sekondari.

Vilevile, Jimbo hili linaendelea kutatua tatizo la UMBALI MREFU wanaotembea Wanafunzi kwenda masomoni mbali na wanakoishi.

## IDADI YA SEKONDARI ZA MUSOMA VIJIJINI

*22 za Kata/Serikali, ikiwemo MPYA (Seka Sekondari) iliyofunguliwa tarehe 5.7.2021
*2 za Binafsi
*10 zinazojengwa au nyingine ujenzi utaanza hivi karibuni

## KATA ISIYOKUWA NA SEKONDARI

Kata ya IFULIFU ndiyo Kata pekee isiyokuwa na Sekondari yake.
Kata hiyo imeamua kujenga SEKONDARI 2 kwa wakati mmoja kwa utaratibu huu:
(i)Kijiji cha Nyasaungu kimeamua kujenga SEKONDARI ya Kijiji chake.
(ii)Vijiji vya Kabegi na Kiemba navyo vinajengwa SEKONDARI ya Vijiji vyao viwili.

**SEKONDARI YA 22 YAFUNGULIWA JIMBONI MWETU**
Kata ya NYAMRANDIRIRA yenye Vijiji 5 (Chumwi, Kaboni, Kasoma, Mikuyu na Seka) ilikuwa na SEKONDARI MOJA tu (Kasoma Sekondari) kwa Wanafunzi wa kutoka Vijiji vyote vitano.

SEKONDARI ya PILI ya Kata hiyo (Seka Sekondari) imefunguliwa tarehe 5.7.2021 ikiwa na WANAFUNZI 113 wa Kidato cha Kwanza na Walimu 7.

**SEKONDARI MPYA YA KATA**
(Seka Sekondari)
WANAFUNZI wa Kidato cha Kwanza wa Kata ya Nyamrandirira kwa sasa wako kwenye SEKONDARI MBILI za Kata yao, yaani, wapo wanaosoma Kasoma Sekondari na wengine wanasoma Seka Sekondari.

Kwa hiyo, MATATIZO ya MIRUNDIKANO ya Wanafunzi madarasani yaliyoko Kasoma Sekondari yameanza kutatuliwa.

Vilevile, WANAFUNZI wa Kidato cha Kwanza wa kutoka Vijiji vya Chumwi, Mikuyu na Seka wamepunguza UMBALI wa kutembea kwenda masomoni.

**MICHANGO YA UJENZI WA SEKONDARI MPYA YA SEKA**
**(**i) WANAVIJIJI:
Wanachangia FEDHA TASLIMU kwa mpangilio huu:
*Kijiji cha Kaboni – kila Kaya inachangia Tsh 10,000/=
*Kijiji cha Seka – kila Kaya inachangia kati ya Tsh 15,000/= na 20,000/=
*Kijiji cha Kasoma – kila Kaya inachangia Tsh 10,000/=
*Kijiji cha Chumwi – kila Kaya inachangia Tsh 6,500/=
*Kijiji cha Mikuyu – kila Kaya inachangia Tsh 20,000/=
*NGUVUKAZI za Wanavijiji wa Vijiji vyote 5 – kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji.

(ii)MADIWANI 2 wa Kata: Mhe Mwl Nyeoja Wanjara na Mhe Mwl Nyachiro Makweba (Viti Maalum) wamechangia jumla ya Tsh 515,000/=

(iii) MGODI wa MMG uliopo Kijijini Seka umechangia:
*Tsh Milioni 8
*Mawe tripu 20
*Molamu tripu 50
*Mchanga tripu 10
*Utengenezaji wa barabara iendayo Seka Sekondari

(iv) WAZALIWA 22 wa Kata ya Nyamrandirira wamechangia jumla ya Tsh 1,930,000/=

(v) MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo amechangia:
Saruji mifuko 250

*MFUKO wa JIMBO umechangia:
Saruji mifuko 450

(vi) HALMASHAURI yetu imechangia:
*Saruji Mifuko 50
*Tsh Milioni 5

(vi) DEO Sekondari, Mwl Majidu Kalugendo amechangia
Tsh 60,000/=

SEKA SEKONDARI imefunguliwa ikiwa na miundombinu ifuatayo:
*Vyumba 3 – Vyumba 2 ni vya Madarasa na Ofisi 1 ya Walimu.
*Matundu 12 ya Vyoo vya Wanafunzi
*Matundu 2 ya Choo cha Walimu

MKUU wa SEKA SEKONDARI, Mwl Isaac Jonathan na VIONGOZI wa Kata na Vijiji vyake vitano, WANAWAOMBA sana WAZALIWA wa VIJIJI vyote 5 vya Kata yao ya NYAMRANDIRIRA, na WADAU wengine wa Maendeleo, waendelee KUJITOKEZA KUCHANGIA UJENZI wa Sekondari hii mpya.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MUSOMA VIJIJINI IMEAMUA KUWA NA "HIGH SCHOOLS" ZA MASOMO YA SAYANSI – KIRIBA SEKONDARI YAKAMILISHA UJENZI WA MAABARA TATU

Posted on July 14, 2021



*MAABARA 3 za Physics, Chemistry na Biology za KIRIBA SEKONDARI iliyoko Kijijini Bwai Kwitururu, Kata ya Kiriba zimekamilika.*

SEKONDARI zetu zote (22) za Kata, na za Binafsi (2) zitakamilisha ujenzi wa MAABARA 3 (Physics, Chemistry and Biology) mwakani (2022).

SEKONDARI mpya (10) zinazojengwa Jimboni mwetu lazima nazo zitajenga MAABARA hizo tatu.

**UAMUZI WA KUWA NA "HIGH SCHOOLS" JIMBONI MWETU**

WANANCHI wa Musoma Vijijini wameamua kuwa na "High Schools" za Masomo ya Sayansi ili kupandisha kiwango cha ELIMU kitolewacho Jimboni mwetu.

Vilevile, maombi ya kujenga CHUO cha UFUNDI (VETA) tayari yameishawasilishwa kwenye Wizara ya Elimu.

VIJANA wanaomaliza Darasa la Saba, na Kidato cha Nne wanazidi KUONGEZEKA Jimboni mwetu. Kwa hiyo, FURSA za KUJIENDELEZA kwa VIJANA hao zinapaswa kuwepo ndani na nje ya Jimbo letu.

**KIRIBA SEKONDARI IMEKAMILISHA UJENZI WA MAABARA TATU ZA SAYANSI**

KIRIBA SEKONDARI ya Kata ya Kiriba yenye Vijiji 3 (Bwai Kumsoma, Bwai Kwitururu na Kiriba) tayari imekamilisha ujenzi wa MAABARA 3 za Physics, Chemistry na Biology.

SEKONDARI hii ilifunguliwa Mwaka 2006 na ina jumla ya Wanafunzi 731 (Form I – IV). Kata ya Kiriba imeanza ujenzi wa Sekondari yake ya pili.

MATAYARISHO ya kuwa na "High School" ya michepuo (combinations) za PCM na PCB yanaendelea kwa kuanza ujenzi wa:
*Bweni la Wanafunzi 70
*Bwalo la Chakula
*Jiko
*Maktaba yenye Kompyuta

**MICHANGO YA UJENZI WA MAABARA HIZO**

*MTENDAJI KATA, Ndugu Pendo Isaac Mwita, MRATIBU ELIMU KATA, Ndugu Beatrice Ndosi, MKUU WA SEKONDARI, Mwl Mtani Paul na VIONGOZI wengine wa Kata na Vijiji vyote 3 wamefanikiwa kuhamasisha na kushawishi WANAVIJIJI kuchangia ujenzi huu.

**WANAVIJIJI**

Wamechangia NGUVUKAZI zao kwa kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya kujengea.

*MBUNGE wa JIMBO, Prof Sospeter Muhongo, mbali ya MICHANGO yake yeye mwenyewe, amefanikiwa kushawishi baadhi ya WAZALIWA wa Kata ya Kiriba kuchangia ujenzi huu.

*BENKI ya CRDB imechangia Tsh MILIONI 20 – Ahsante sana CRDB!

MICHANGO inaombwa ya kuchangia ujenzi ulioelezwa hapo juu kwa lengo la kuwa na "HIGH SCHOOL" ya michepuo ya PCM na PCB mwakani (Julai 2022). MICHANGO ipelekwe kwa Mkuu wa Shule au Mtendaji Kata.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# ELIMU MUSOMA VIJIJINI: LENGO JIPYA NI KUWA NA "HIGH SCHOOLS" ZA MASOMO YA SAYANSI KUANZIA MWAKANI (2022)

Posted on July 12, 2021



*MAABARA ya Chumba kimoja (Kemia) inayokamilishwa hapo MAKOJO SEKONDARI ya Kata ya Makojo.*

JIMBO la Musoma Vijijini lina VIPAUMBELE 5 ambavyo vinatokana na ILANI za UCHAGUZI za CCM (2020-2025, 2015-2020 & 2010-2015)

VIPAUMBELE hivyo vitano (5) ni:
*Elimu
*Afya
*Kilimo, Uvuvi na Ufugaji
*Tabianchi na Mazingira
*Michezo na Utamaduni

**KIPAUMBELE CHA ELIMU**
JIMBO linaendelea kujenga na kuboresha MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye Shule za Msingi na Sekondari.

Tunazo Kata 21 zenye jumla ya Vijiji 68 na Vitongoji 374.

**IDADI YA SHULE ZA SEKONDARI**
“SECONDARY SCHOOLS (Form I – IV)”
*Sekondari za Kata/Serikali: 22
*Sekondari za Binafsi: 2
*Sekondari Mpya zinazojengwa: 10

**“HIGH SCHOOLS (Form V – VI)”**
*Tunayo moja tu, Kasoma High School, yenye michepuo (combinations) za HGK, HGL na HKL.

**UJENZI NA UBORESHAJI WA MAABARA KWENYE SEKONDARI ZETU**
SEKONDARI 22 za Kata za Jimboni mwetu zinaendelea na ujenzi na uboreshaji wa MAABARA zinazohitajika kwenye Masomo ya Sayansi. MAABARA hizo ni za masomo ya Fizikia, Kemia na Biolojia.

Vilevile, MAABARA za Masomo ya Sayansi zinajengwa kwenye Sekondari zetu mpya.

**KUANZISHWA “HIGH SCHOOLS” ZA MASOMO YA SAYANSI**
LENGO letu jipya ni mwakani (2022) kuwa na “High Schools” za Masomo ya Sayansi yenye michepuo (combinations) iliyowekwa na Serikali.

Kwa hiyo, WANAVIJIJI kwa kushirikiana na SERIKALI, na WADAU wengine wa MAENDELEO, wanaendelea KUJITOLEA kujenga MAABARA za SAYANSI za KISASA kwenye Sekondari zao za Kata.

**MFANO WA MAABARA ZINAZOJENGWA MUSOMA VIJIJINI**
***MAKOJO SEKONDARI**
SEKONDARI hii ni ya Kata ya Makojo. Ilifunguliwa Mwaka 2006 na ina Wanafunzi 423. Kata ya Makojo ina Vijiji 3, ambavyo ni Chimati, Chitare na Makojo

*WANAKIJIJI wamechangia Matofali 1,300; na wamesomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi (NGUVUKAZI)

DIWANI VITI MAALUM, Mhe Tabu Machumu anafanya kazi nzuri ya kuchangia na kuhamasisha ujenzi huu akishirikiana na Mtendaji Kata, Ndugu Peresi Mgaya.

MKUU wa Makojo Sekondari, Mwl Emmanuel Daghau, amesimamia vizuri matumizi ya Tsh MILIONI 30 zilizotolewa na SERIKALI kwa ajili ya ukamilishaji wa CHUMBA 1 cha MAABARA ya Kemia.

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo ameahidi kuchangia MABATI 53 yatakapohitajika kuezeka Chumba cha Maabara ya pili.

VITABU vya Masomo ya SAYANSI: Mbunge wa Jimbo ataendelea kuleta VITABU vingi vya masomo ya SAYANSI kutoka USA na UK, na kuvigawa bure mashuleni mwetu.

KARIBUNI tuchangie ujenzi na uboreshaji wa MAABARA za Sekondari zetu ikiwa ni MAANDALIZI ya kuwa na "HIGH SCHOOLS" za masomo ya SAYANSI Jimboni mwetu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAKTABA NA MAABARA ZAENDELEA KUJENGWA

Posted on January 5, 2022



*MAKTABA ya Shule ya Msingi Karubugu, Kijijini Kurwaki IMEKAMILIKA*

MAKTABA ya Shule ya Msingi Karubugu, Kijijini Kurwaki IMEKAMILIKA

**MICHANGO YA UJENZI WA MAKTABA HIYO**

*Wanakijiji wamechangia nguvukazi na fedha taslimu. Daftari linaloonyesha MICHANGO iliyotolewa liko kwenye Serikali ya Kijiji cha Kurwaki.

*WANAFUNZI na WAKAZI wengine wa Vijiji vya Kurwaki na Kiriba, na Viongozi wa Kata zao WANAISHUKURU sana PCI TANZANIA na MBUNGE wao wa Jimbo Prof Muhongo kwa KUTOA MICHANGO MIKUBWA kukamilisha UJENZI wa MAKTABA ya Shule yao ya Msingi.

Wanafunzi wa S/M Karubugu wanatoka Vijiji vya Kurwaki (Kata ya Mugango) na Kiriba (Kata ya Kiriba)

VITABU vya MAKTABA hiyo vimetolewa na PCI TANZANIA na MBUNGE wao Prof Sospeter Muhongo.

Mbunge huyo ataongenezea VITABU kwenye Maktaba hiyo.

MATUMIZI ya MAKTABA ILIYOJENGWA & KUKAMILIKA
*Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari wanakaribishwa
*Walimu wa shule za Msingi na Sekondari wanakaribishwa.
*Wakazi wa Vijiji na Kata za jirani wanakaribishwa.

**UJENZI WA MAKTABA NA MAABARA ZA SAYANSI KWENYE SHULE ZA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI UNAENDELEA.**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM WAJENGEWA VYUMBA VIPYA 2 VYA MADARASA NA OFISI 1 YA WALIMU

Posted on August 4, 2021



*Hatua iliyofikiwa kwenye ujenzi wa VYUMBA VIPYA vya Madarasa na OFISI ya Walimu kwenye S/M NYAMBONO B yenye Wanafunzi wenye MAHITAJI MAALUM*

WANAFUNZI wenye Mahitaji Maalumu wanajengewa Vyumba viwili (2) vya Madarasa na Ofisi moja (1) ya Walimu kwenye Shule wanayosoma, S/M NYAMBONO B, Kijijini Saragana.

Kijiji cha Saragana kina Shule 2 za Msingi, ambazo ni S/M Nyambono na S/M Nyambono B. Kijiji hiki ni kimoja kati ya Vijiji 2 (Nyambono & Saragana) vya Kata ya Nyambono.

KAIMU MWALIMU MKUU wa S/M Nyambono B, Mwl Salum Abdalah ameelezea yafuatayo kuhusu Shule hiyo:
*Ilifunguliwa Mwaka 2010 na ina jumla ya Wanafunzi 809.
*Wanafunzi 22 ni wale wenye Mahitaji Maalum (wenye matatizo mbalimbali ya kiafya).
*Shule hii ina Walimu 9, kati ya hao, Walimu wawili (2) wanafundisha Wanafunzi 22 wenye Mahitaji Maalum.
*Vyumba vya Madarasa vinavyohitajika ni 12, vilivyopo 4
*Matundu 32 ya Vyoo yanahitajika, yaliyopo ni 8
*Choo cha Walimu chenye Matundu 2 kipo.
*Zinahitajika nyumba 9 za Walimu, ipo 1 tu.

**UFAULU WA MITIHANI WA S/M NYAMBONO B**
*DARASA la IV (2020)
Watahiniwa: 89
Waliofaulu: 89

*DARASA la VII (2020)
Watahiniwa: 58
Waliofaulu: 48

**WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM WAJENGEWA MADARASA**
MWALIMU KIONGOZI wa Kitengo cha Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum, MWL ABEID PAUL ameelezea YAFUATAYO kuhusu hali za Wanafunzi hao:

*Wanafunzi wenye ulemavu kwenye ubongo (intellectual impairment) ni 16

*Wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia (hearing impairment) ni 6

**MICHANGO KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM**
SHIRIKA la BMZ la UJERUMANI linatoa MISAADA mingi kwa Wanafunzi hao ikiwemo:

*Vifaa vya Shule mbalimbali, k.m. mabegi, madaftari na kalamu

*Matibabu ya bure, yakiwemo ya upasuaji (operations) kwenye Hospitali Teule ya Shirati.

*Ofisi ya Miradi ya SHIRIKA la BMZ ipo Hospitali Teule ya Shirati

*Vifaa Maalum vya (kimatibabu) vinavyohitajika, k.m. baiskeli maalum, miwani, vifaa vya kuongeza usikivu, fimbo maalum za kutembelea na miguu bandia

**AHSANTE SANA SANA BMZ (Ujerumani)**

**WACHANGIAJI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU YA S/M NYAMBONO B**

**(i) WANAKIJIJI:**

Wanachangia NGUVUKAZI za kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi.

**(ii)SERIKALI YA KIJIJI:**

Mapato ya ndani (20%) ya Serikali ya Kijiji cha Saragana yanachangia ujenzi huu.

**(iii)TASAF:**

*Ujenzi wa Vyumba 2 vya Madarasa na Madawati 32
*Vifaa vya Shule (mabegi, madaftari na kalamu)
kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

**(iv)MBUNGE wa JIMBO:**

Prof Sospeter Muhongo amechangia kama ifuatavyo:
*Madawati 75
*Vitabu zaidi ya 1,000 vya Maktaba

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA SARAGANA**

MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Saragana, Ndugu Ernest Jama Kamori anawaomba WAZALIWA wa Kijiji cha Saragana, na WADAU wengine wa MAENDELEO wajitokeze KUCHANGIA ujenzi na ukamilishaji wa MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye Shule zao za Msingi na Sekondari zilizopo Kijijini hapo.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijiji
www.musomavijijini.or.tz

# SHULE YA MSINGI KAMBARAGE YAENDELEA KUJENGA NA KUBORESHA MIUNDOMBINU YAKE YA ELIMU

Posted on July 31, 2021



*Ujenzi wa Vyumba vipya viwili vya Madarasa na Ofisi moja ya Walimu unaoendelea kwenye S/M KAMBARAGE ya Kijijini Kakisheri, Kata ya Nyakatende.*

SHULE ya MSINGI KAMBARAGE iko Kijijini Kakisheri, Kata ya Nyakatende.

KIJIJI cha Kakisheri kina jumla ya KAYA 542 na Wakazi wake ni 1,047. Kijiji hiki kina shule moja tu ya Msingi (S/M Kambarage) iliyofunguliwa Mwaka 2001.

MWALIMU MKUU wa S/M Kambarage, Mwl Gerlad Wanyaka ameelezea yafuatayo kuhusu Shule hii:
*Jumla ya Wanafunzi ni 710.
*Idadi ya Walimu wanaohitajika ni 15, waliopo ni 7
*Vyumba vya Madarasa vinavyohitajika ni 16, vilivyopo ni 8
*Idadi ya matundu ya CHOO yanayohitajika ni 22, yaliyopo ni 15
*Nyumba za Walimu zinazohitajika ni 15, zilizopo ni 3.
*Mirundikano ya Wanafunzi Madarasani ni mikubwa, mifano:

(i) Wanafunzi 121 wa Darasa la Awali wanatumia chumba kimoja cha darasa.
(ii) Wanafunzi 112 wa Darasa la VI wanatumia chumba kimoja cha darasa.

**MICHANGO YA WANAKIJIJI KWENYE UJENZI WA VYUMBA VIPYA 2 VYA MADARASA NA OFISI 1 YA WALIMU**
MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Kakisheri, Ndugu Maridadi Magafu ameeleza yafuatayo kuhusu ushiriki wa WANAKIJIJI kwenye ujenzi huo:

***WANAKIJIJI:**
(i) Kuchimba Msingi wa Vyumba vipya 2 vya Madarasa na Ofisi 1 ya Walimu
(ii) Kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi
(iii) Michango ya FEDHA taslimu SHILINGI 4,200/= kutoka kwa kila MKAZI wa Kijiji hicho mwenye umri wa zaidi ya miaka 18.

**MICHANGO MINGINE ILIYOKWISHATOLEWA KWENYE S/M KAMBARAGE**
*MBUNGE wa Jimbo, Profesa Sospeter Muhongo ameshachangia:
(i) Madawati 100
(ii) Saruji Mifuko 60
(iii) Mabati 54
(iv) Vitabu zaidi ya 1,000 vya Maktaba

***MFUKO WA JIMBO umechangia**
(v) Saruji Mifuko 100

*MDAU wa MAENDELEO, Ndugu Mauza Nyakirang'anyi, alichangia MBAO za KUPAUA Chumba 1 cha Darasa.

**UFAULU WA MITIHANI WA S/M KAMBARAGE**
*MATOKEO Darasa la IV (2020)
Watahiniwa: 86
Waliofaulu: 82

*MATOKEO Darasa la VII (2020)
Watahiniwa: 50
Waliofaulu: 49

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA KAKISHERI**

*UONGOZI na WANAKIJIJI wanatoa wito kwa WAZALIWA wa Kijiji cha Kakisheri na Kata ya Nyakatende kwa ujumla wake, na WADAU wengine wa MAENDELEO kujitokeza kuchangia ujenzi na uboreshaji wa MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye S/M KAMBARAGE – karibuni tuendelee kumuenzi BABA wa TAIFA kwa pamoja.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SHULE YA MSINGI ILIYOFUNGULIWA MWAKA 1942 YAPATA MCHANGO WA SERIKALI WA KUTATUA TATIZO LA UKOSEFU WA VYUMBA VYA MADARASA

Posted on July 31, 2021



*Ujenzi wa Vyumba Vipya viwili vya Madarasa na Ofisi moja ya Walimu unaoendelea kwenye S/M BULINGA ya Kijijini Bugunda, Kata ya Bwasi.*

KIJIJI cha BUGUNDA kilichoko Kata ya Bwasi kina SHULE MBILI za MSINGI – S/M Bulinga na S/M Bulinga B

MWALIMU MKUU wa S/M Bulinga, Mwl Alexander Materu ameeleza yafuatayo kuhusu Shule hiyo:
*Ilifunguliwa Mwaka 1942 na kwa sasa ina jumla ya Wanafunzi 662
*Idadi ya Walimu wanaohitajika ni 15, waliopo ni 7
*Vyumba vya Madarasa vinavyohitajika ni 14, vilivyopo ni 6
*Mirundikano ya Wanafunzi madarasani ni mikubwa sana, kwa mfano, Wanafunzi 147 wa Darasa la III wanatumia chumba kimoja cha darasa.
*Jumla ya WANAFUNZI 214 wanasomea nje, chini ya miti.

## MCHANGO WA SERIKALI WA KUTATUA TATIZO LA UKOSEFU WA VYUMBA VYA MADARASA

*SERIKALI kupitia Mradi wake wa EP4R imetoa SHILINGI MILIONI 40 kwa ajili ya kukamilisha Vyumba vipya viwili vya Madarasa, Ofisi 1 ya Walimu na ununuzi wa Madawati.

**MICHANGO YA WANAKIJIJI KWENYE UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA YA SHULE YAO**
*MTENDAJI KATA, Ndugu Mashaka Kagere amesema WANAKIJIJI wanashiriki katika ujenzi huo kwa kufanya yafuatayo:
(i) Kuchimba Msingi wa Vyumba vipya 2 vya Madarasa na Ofisi 1 ya Walimu
(ii) Kusomba mawe, mchanga na maji ya ujenzi

**MICHANGO MINGINE ILIYOKWISHATOLEWA KWENYE S/M BULINGA**
*PCI Tanzania ilijenga Matundu 8 ya Choo cha Wanafunzi
*MBUNGE wa Jimbo, Profesa Sospeter Muhongo ameshachangia:
(i) Madawati 46
(ii) Vitabu zaidi ya 1,000 vya Maktaba

***MFUKO wa JIMBO umechangia**
(iii) Mabati 54

*Halmashauri yetu ilishachangia Shilingi Milioni 5.

**UFAULU WA MITIHANI WA S/M BULINGA**
*MATOKEO Darasa la IV (2020)
Watahiniwa 85
Waliofaulu 85

*MATOKEO Darasa la VII (2020)
Watahiniwa 32
Waliofaulu 31

**SHUKRANI KUTOKA KIJIJI CHA BUGUNDA**
*Wanakijiji na Viongozi wao wanaishukuru sana SERIKALI kwa MCHANGO wake wa SHILINGI MILIONI 40.

**OMBI KUTOKA KIJIJI CHA BUGUNDA**
*WAZALIWA wa Kijiji cha Bugunda na Kata ya Bwasi kwa ujumla wake, na WADAU wengine wa MAENDELEO wanaombwa wachangie ujenzi wa MIUNDOMBINU ya ELIMU ya SHULE KONGWE (S/M Bulinga) iliyofunguliwa Mwaka 1942.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAVIJIJI WASHIRIKIANA NA SERIKALI KUTATUA TATIZO LA UPUNGUFU WA VYUMBA VYA MADARASA MASHULENI

Posted on July 10, 2021



*Ukamilishaji wa ujenzi wa Vyumba vipya vya Madarasa vya S/M NYASAUNGU iliyoko Kijijini Nyasaungu, Kata ya Ifulifu.*

JIMBO la Musoma Vijijini laendelea kuongoza kwenye UTEKELEZAJI wa ILANI za UCHAGUZI za CCM (2020-2025 & 2015-2020)

**MATATIZO YA UPUNGUFU WA VYUMBA VYA MADARASA**
**SHULE ZA MSINGI**
*Vyumba vipya 380 vimejengwa na kukamilika
*Maboma 50 ya Vyumba vipya vya Madarasa yanakamilishwa ujenzi

**SHULE ZA SEKONDARI**
*Vyumba vipya 78 vya Madarasa vimejengwa na kukamilika
*Maboma 25 ya Vyumba vipya vya Madarasa yanakamilishwa ujenzi

**SHULE ya MSINGI NYASAUNGU**
KIJIJI cha Nyasaungu ni kimoja kati ya Vijiji 3 (Kabegi, Kiemba na Nyasaungu) vya Kata ya IFULIFU

KIJIJI cha Nyausungu chenye VITONGOJI vitano (5) kina WAKAZI wapatao 315, na kina Shule moja ya Msingi ijulikanayo kwa jina la SHULE ya MSINGI NYASAUNGU

KAIMU MWALIMU MKUU wa Shule hii, Mwl Stephen Musibha ameeleza yafuatayo kuhusu Shule hiyo:
*Ilianzishwa Mwaka 1999 na kwa sasa inao Wanafunzi 788
*Mahitaji ya vyumba vya Madarasa ni 14, vilivyopo ni 8
*Darasa la Tatu ndilo lenye MRUNDIKANO mkubwa wa WANAFUNZI darasani, Wanafunzi 131 wanasomea kwenye chumba kimoja cha Darasa.
*Matundu ya Vyoo yanayohitajika ni 39, yapo 8 tu.
*Mahitaji ya Walimu ni 15, waliopo ni 5 tu
*Nyumba 15 za Walimu zinahitajika, zipo 5 za Walimu watano (5) waliopo

**MICHANGO YA UJENZI WA VYUMBA VIPYA VYA MADARASA VYA S/M NYASAUNGU**
MWENYEKITI wa Serikali ya Kijiji cha Nyasaungu, Ndugu Magesa Chacha Marera amebainisha MICHANGO inayoendelea kutolewa kama ifuatavyo:

***WANAKIJIJI**
(i) NGUVUKAZI za kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya kujengea
(ii) Kila Kitongoji kinachangia Tsh 107,000 au Matofali 40 kwa kila awamu ya ujenzi

*SERIKALI, kupitia Mradi wake wa EP4R, imechangia SHILINGI MILIONI 12 kupaua Chumba kimoja cha Darasa na Ofisi moja ya Walimu. Shukrani nyingi kwa SERIKALI yetu.

**MICHANGO MINGINE ILIYOTOLEWA KWENYE S/M NYASAUNGU**
*PCI Tanzania
imejenga Matundu 8 ya Vyoo vya Wanafunzi. Shukrani nyingi sana kwa PCI Tanzania.

*PCI Tanzania inachimba Kisima cha Maji cha S/M Nyasaungu. Ahsanteni sana PCI Tanzania.

***MBUNGE WA JIMBO**
Prof Sospeter Muhongo amechangia:
(i) Saruji Mifuko 50
(ii) Madawati 130
(iii) Vitabu zaidi ya 1,000 vya Maktaba

***MFUKO WA JIMBO umechangia**
(i) Mabati 108

**MATOKEO YA MITIHANI YA TAIFA YA S/M NYASAUNGU DARASA LA IV (2020)**
*Watahiniwa: 92
*Waliofaulu: 92

**DARASA LA VII (2020)**
*Watahiniwa: 40
*Waliofaulu: 31

**OMBI KUTOKA KIJIJINI NYASAUNGU**
*KIJIJI hiki kinayo MIRADI mikuu mitatu (3) inayotekelezwa kwa sasa. MIRADI hiyo ni ya ujenzi wa SEKONDARI ya Kijiji, ZAHANATI ya Kijiji na VYUMBA VIPYA vya Madarasa kwenye Shule yao ya Msingi.

*WAZALIWA wa Kijiji cha Nyasaungu wanaombwa kujitokeza kuchangia MAENDELEO ya Kijijini KWAO. WADAU wa MAENDELEO nao wanakaribishwa.

**Karibuni sana tuchangie MAENDELEO ya Kijiji cha NYASAUNGU**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI LAFURAHISHWA KUWEPO KWA FEDHA ZA IMF KWA AJILI YA KUKAMILISHA UJENZI WA SHULE SHIKIZI

Posted on October 12, 2021



*Baadhi ya majengo yaliyokamilika katika SHULE Shikizi NYASAENGE, Kijijini Kataryo, Kata ya Tegeruka*

SHULE SHIKIZI zinazojengwa na baadae kupanuliwa kuwa SHULE za MSINGI kamili zitakazojitegemea ni kumi na mbili (12). SHULE hizo ni:

1. Shule shikizi Binyago: Kijiji cha Kabegi, Kata ya Ifulifu
2. Shule shikizi Buanga: Kijiji cha Buanga, Kata ya Rusoli
3. Shule shikizi Buraga: Kijiji cha Buraga, Kata ya Bukumi
4. Shule shikizi Egenge: Kijiji cha Busamba, Kata ya Etaro
5. Shule shikizi Gomora: Kijiji cha Musanja, Kata ya Musanja
6. Shule shikizi Kaguru: Kijiji cha Bugwema, Kata ya Bugwema
7. Shule shikizi Karusenyi: Kijiji cha Mikuyu, Kata ya Nyamrandirira
8. Shule shikizi Kiunda: Kijiji cha Kamguruki, Kata ya Nyakatende
9. Shule shikizi Mwikoko: Kijiji cha Chitare, Kata ya Makojo
10. Shule shikizi Nyasaenge: Kijiji cha Kataryo, Kata ya Tegeruka
11. Shule shikizi Rwanga: Kijiji cha Kasoma, Kata ya Nyamrandirira
12. Shule shikizi Ziwa: Kijiji cha Mwiringo, Kata ya Busambara

***WACHANGIAJI WA UJENZI WA SHULE SHIKIZI NDANI YA JIMBO LETU**

**SERIKALI KUU**

*Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanashukuru sana kwa kupokea MICHANGO MINGI kutoka SERIKALI KUU (k.m. TAMISEMI) kwa ajili ya UJENZI na UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU ya ELIMU kwenye shule zetu zote za Jimboni mwetu.

**WANANCHI**

*Huchangia NGUVUKAZI za kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi

*Huchangia fedha taslimu kutoka kila kaya

**MADIWANI**

*Madiwani wanashirikiana na Wanavijiji kuchangia miradi ya ujenzi iliyoko kwenye Kata zao.

**MBUNGE WA JIMBO**

Prof Sospeter Muhongo, Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini ni mchangiaji mkubwa wa UJENZI na UBORESHAJi wa Miundombinu ya Elimu kwenye SHULE zote SHIKIZI, MSINGI na SEKONDARI za Jimboni mwetu.

**MFUKO WA JIMBO**

*Iliamuliwa kwamba Fedha za Mfuko wa Jimbo, chini ya Mwenyekiti wake, Mbunge wa Jimbo, zitumike kwenye Miradi ya ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu ya Elimu ya shule zetu. Hayupo anayepewa fedha mkononi. Halmashauri hununua vifaa vya ujenzi na kuvigawa kama ilivyopangwa.

**WAZALIWA WA MUSOMA VIJIJINI**

Baadhi yao huchangia miradi ya ujenzi ya Vijijini kwao. Majina yao hutajwa kwenye Ripoti za Ofisi ya Mbunge.

**WADAU WENGINE WA MAENDELEO**

Jimbo letu linashukuru sana kupata WADAU wa MAENDELEO (k.m. Benki za nchini mwetu, PCI Tanzania, BMZ Ujerumani) ambao wanachangia ujenzi na uboreshaji wa Miundombinu ya Elimu ya shule zetu. Na wao pia majina yao hutajwa kwenye Ripoti za Ofisi ya Mbunge

**HALMASHAURI YETU**

Ushauri umetolewa kwa Halmashauri yetu ICHANGIE IPASAVYO, na kwa UWAZI, kwenye Miradi ya Maendeleo ya Wanavijiji wa Jimboni mwetu.

**JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI LIKO TAYARI KUANZA KUTUMIA FEDHA ZA IMF**

MAKUSUDIO ya matumizi ya FEDHA za IMF yanaoana vizuri sana na MIRADI inayotekelezwa kwa sasa Jimboni mwetu.

TUNAJENGA SHULE SHIKIZI 12, ambazo zimetajwa hapo juu na tunatoa hapa MIFANO MIWILI kushawishi FEDHA za IMF zichangie Miradi yetu ya ujenzi wa SHULE SHIKIZI za Jimboni mwetu

**SHULE SHIKIZI NYASAENGE, KIJIJINI KATARYO, KATA YA TEGERUKA**

Hapo awali, Wanafunzi wa Kitongoji cha Nyasaenge walilazimika kutembea umbali wa zaidi ya Kilometa 10 kwenda masomoni kwenye Shule za Msingi za KATARYO na KATARYO B.

SHULE SHIKIZI hii imekamilisha Vyumba vipya 2 vya Madarasa na Ofisi 1 ya Walimu. Darasa la Awali lina Wanafunzi 106. Ujenzi unaendelea.

**SHULE SHIKIZI GOMORA, KIJIJINI MUSANJA, KATA YA MUSANJA**

Wanafunzi wa Kitongoji cha GOMORA wanalazimika kwenda masomoni kwenye Shule za Msingi jirani za Lyasembe (Kata ya Murangi), na Bwenda (Kata ya Rusoli). Ujenzi wa SHULE SHIKIZI GOMORA unaendelea.

**UPATIKANAJI WA FEDHA ZA IMF: PONGEZI NYINGI SANA ZINATOLEWA KWENYE SERIKALI YETU CHINI YA UONGOZI MZURI WA MHE DKT RAIS SAMIA SULUHU HASSAN**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WAKAZI WA KITONGOJI CHA GOMORA WAJENGA SHULE MPYA KUONDOKANA NA ADHA WANAYOPATA WATOTO WAO YA KWENDA MBALI MASOMONI

Posted on September 29, 2021



*Ujenzi unaoendelea wa vyumba vipya 2 vya Madarasa na Ofisi 1 ya Walimu ya Shule Shikizi ya Kitongoji cha Gomora, Kijijini Musanja Kata ya Musanja*

Jimbo la Musoma Vijijini kwa sasa linajenga SHULE MPYA ZA MSINGI 12 (Shule Shikizi 12) ili kutatua matatizo sugu mawili ambayo ni:
*Umbali mrefu wanaotembea Wanafunzi kwenda masomoni (umbali wa zaidi ya kilomita 4)
*Mirundikano ya Wanafunzi kwenye vyumba vya madarasa (Wanafunzi zaidi ya 45)

SHULE SHIKIZI 12 zinazojengwa ni: Binyago, Buanga, Buraga, Egenge, Gomora, Kaguru, Karusenyi, Kiunda, Mwikoko, Nyasaenge, Rwanga na Ziwa.

SHULE ZA MSINGI zilizopo ni:
*111 za Serikali
*3 za Binafsi

**KITONGOJI CHA GOMORA**
Kata ya Musanja ina Vijiji vitatu ambavyo ni Musanja, Nyabaengere na Mabui Merafuru.

Wakazi wa Kitongoji cha Gomora kilichopo Kijiji cha Musanja wameanza ujenzi wa shule mpya ili kuondokana na adha ya watoto wao kutembea umbali mrefu kwenda masomoni kwenye S/M MUSANJA.

MWALIMU MKUU, Mwl Ngasa Msabi ameeleza kuwa Kijiji cha Musanja kina Shule moja ya Msingi ambayo ni S/M MUSANJA iliyofunguliwa Mwaka 1956, kwa sasa ina:
*Wanafunzi 815
*Walimu 8, Pungufu 10
*Vyumba 7 vya Madarasa, Pungufu 12

WANAFUNZI wa KITONGOJI cha GOMORA wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya KILOMITA 4 kwenda masomoni kwenye S/M Musanja.

Wengine wanatembea umbali mrefu zaidi kwenda masomoni kwenye Shule za Msingi jirani za Lyasembe (Kata ya Murangi), na Bwenda (Kata ya Rusoli).

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Gomora, Ndugu Sospeter Mjarifu ameeleza kuwa WANAKIJIJI wa Kitongoji hicho wameamua kujenga shule yao kwa kutumia MICHANGO ya WANAKIJIJI, DIWANI wa KATA, MBUNGE wa JIMBO na WADAU wengine wa MAENDELEO.

**HADI SASA MICHANGO imetolewa na:**
***WANAKIJIJI:**
(i) kuchimba msingi wa Vyumba vipya 2 vya Madarasa na Ofisi 1 ya Walimu
(ii) kusomba mawe, mchanga na maji ya ujenzi
(iii) kuchangia fedha taslimu, Tsh 15,000/= kutoka kila Kaya

***DIWANI WA KATA:**
Ndugu Ernest Mwira alitayarisha HARAMBEE ambayo yeye na WADAU wa MAENDELEO wamechangia:
(i) Fedha Taslimu Tshs1.3 Milioni
(ii) Mifuko ya Saruji 63 na Nondo 8

***MBUNGE WA JIMBO:**
Prof Sospeter Muhongo ameanza kuchangia ujenzi huu kwa kutoa SARUJI MIFUKO 50.

**LENGO KUU LA WANAKIJIJI:**
“Shule Shikizi Gomora ifunguliwe Januari 2022

OMBI kutoka Kitongoji cha Gomora ni kupata MICHANGO kutoka Halmashauri yetu na kutoka kwa Wadau wengine wa Maendeleo kukamilisha ujenzi wa SHULE SHIKIZI GOMORA.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# ELIMU NI KIPAUMBELE MUHIMU SANA CHA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI – VITONGOJI VYAAMUA KUJENGA SHULE SHIKIZI

Posted on September 1, 2021



*Ujenzi wa SHULE SHIKIZI ya KITONGOJI cha BURAGA MWALONI, Kijijini Buraga, Kata ya Bukumi.*

**TAKWIMU MUHIMU:**
Jimbo la Musoma Vijijiji lina:
*Kata 21 zenye Vijiji 68 na Vitongoji 374
*Shule za Msingi 111 za Serikali
*Shule za Msingi 3 za Binafsi
*Sekondari 22 za Kata/Serikali
*Sekondari 2 za Binafsi
*High School 1 ya Serikali ya Masomo ya "Arts"

**MATATIZO YANAYOTATULIWA KWENYE SEKTA YA ELIMU**
WANAVIJIJI wakishirikiana na SERIKALI, na WADAU mbalimbali wa MAENDELEO wanaendelea kutatua matatizo yafuatayo:
*Umbali mrefu wa Wanafunzi kutembea waendapo masomoni.
*Mirundikano ya Wanafunzi kwenye Vyumba vya Madarasa

**UJENZI NA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU**
MIRADI inayoendelea Jimboni mwetu:
*Ujenzi wa Maabara 3 za Fizikia, Kemia na Biolojia kwenye Sekondari zote 22 za Kata/Serikali

*Ujenzi wa Vyumba vipya vya Madarasa, Maktaba, Ofisi za Walimu, Vyoo na Nyumba za Walimu kwenye shule zetu.
*Ujenzi wa Sekondari mpya 10. Hatua mbalimbali zimefikiwa
*Ujenzi wa Shule Shikizi 12, ambazo zitapanuliwa na kuwa Shule za Msingi zinazojitegemea.

**KITONGOJI CHA BURAGA MWALONI CHAANZA UJENZI WA SHULE SHIKIZI**

KITONGOJI cha Buraga Mwaloni kipo Kijiji cha Buraga, Kata ya Bukumi. Kata hii inavyo Vijiji vingine vitatu (Bukumi, Buira na Busekera)

KIJIJI cha Buraga kina Shule moja ya Msingi (S/M Buraga) ambayo ina:
*Wanafunzi 690
*Walimu 10
*Vyumba 8 vya Madarasa
*Ilifunguliwa Mwaka 1978

Hayo yameelezwa na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Mwl Joseph Paul

WANAFUNZI wa Kitongoji cha Buraga Mwaloni WANALAZIMIKA kutembea zaidi ya KILOMITA 5 kwenda masomoni kwenye S/M BURAGA. Vichaka vyenye wanyama wakali ni hatari kubwa kwa Wanafunzi hao!

Wengine wanatembea umbali mrefu kwenda masomoni kwenye S/M CHITARE ya Kijiji cha jirani cha Chitare cha Kata jirani ya Makojo.

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Buraga Mwaloni, Ndugu Steven Wanjara ameeleza kuwa KITONGOJI KIMEAMUA kujenga SHULE SHIKIZI yake na MICHANGO ya ujenzi inatolewa kama ifuatavyo:

**WANA-KITONGOJI:**
*Nguvukazi za kuchimba msingi wa Vyumba 2 vya Madarasa na Ofisi 1 ya Walimu
*Nguvukazi za kusomba mawe, mchanga na maji

*Fedha taslimu, Tsh 19,300/= kutoka kila Kaya

**DIWANI WA KATA**:
Mhe Munubi Musa ameanza kutoa MICHANGO yake kwa kuchangia Tsh 100,000/= (laki moja)

**MBUNGE WA JIMBO:**
Prof Sospeter Muhongo ameanza kwa kuchangia:
*Saruji Mifuko 55
*MFUKO wa JIMBO umechangia Saruji Mifuko 50.

OMBI LA MICHANGO linatolewa na Kitongoji cha Buraga Mwaloni kisaidiwe VIFAA vya UJENZI kukamilisha SHULE SHIKIZI yake – Wanafunzi 40 wa Darasa la Awali wanasomea chini ya miti. HALMASHAURI yetu nayo inapaswa kuchangia ujenzi huu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI
# WA
# MIRADI
# YA
# AFYA
## (30 Juni 2022 – 1 Julai 2021)

**Tarehe 30 Juni 2022: Huduma za Afya Jimboni mwetu:**
*Hospitali ya Wilaya 1: ujenzi unaendelea
*Vituo vya Afya: 3 vinatoa huduma & 3 vinajengwa
*Zahanati: 23 Serikali & 4 Binafsi zinatoa huduma. 15 zinajengwa
*Magari ya Wagonjwa (Ambulances): 5 yanatoa huduma

# SERIKALI YAENDELEA KUSHIRIKIANA NA WANAVIJIJI KWENYE UJENZI WA VITUO VIPYA VYA AFYA VYA MUSOMA VIJIJINI

Posted on June 14, 2022



*Ujenzi unaoendelea wa Kituo kipya cha Afya cha Kata ya Makojo kinachojengwa Kijijini Makojo.*

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 zenye jumla ya Vijiji 68, lina Kata 3 zenye Vituo vya Afya vinavyofanya kazi. Vituo hivyo ni vya:
*Murangi
*Mugango
*Bugwema

Serikali inaendelea kutoa fedha kwenye ujenzi wa Vituo vipya vya Afya, ambavyo ni:
*Kisiwa cha Rukuba
*Makojo
*Kiriba

Kwenye ujenzi huo, Serikali ilitoa Tsh milioni 250 kwa kila Kituo cha Afya kipya kuanza ujenzi wake.

Serikali imetoa tena Tsh milioni 250 kuendeleza ujenzi wa Vituo hivyo vipya. Fedha hizo za awamu ya pili zitapelekwa kwenye Kata husika siku chache zijazo.

Mchango wa Tsh milioni 500 kwa kila Kituo Kipya kinachojengwa Jimboni mwetu ni mchango mkubwa. Tunaishukuru sana Serikali yetu na kipikee kabisa tunamshukuru sana Rais wetu, Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha fedha za utekelezaji wa miradi hii na mingine zinapatakina – Ahsante sana!

Jumla ya ZAHANATI zinazotoa huduma za Afya Jimboni mwetu ni:

*23 za Serikali
*4 za Binafsi

Jumla ya ZAHANATI mpya zinazojengwa ni:

*15 zinajengwa na WANAVIJIJI na baadhi zimepokea michango ya fedha kutoka Serikalini.

MICHANGO ya NGUVUKAZI za WANAVIJIJI inaombwa iendelee kutolewa hadi kukamilika kwa ujenzi wa VITUO VIPYA VYA AFYA na ZAHANATI zinazojengwa.

Usisahau kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni:
www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## KITUO CHA AFYA MAKOJO – WANAVIJIJI WAAMUA KUONGEZA KASI YA UJENZI

Posted on February 11, 2022



*Maboma ya OPD na MAABARA ya KITUO cha AFYA cha Kata ya Makojo kinachojengwa Kijijini Makojo.*

Kwa Mwaka huu wa Fedha, 2021/2022, Jimbo la Musoma Vijijini linajenga VITUO 3 vya AFYA:
*Makojo: chanzo cha fedha – RUZUKU ya Serikali
*Rukuba (Kisiwa): chanzo cha fedha – TOZO
*Kiriba: chanzo cha fedha- TOZO

*VITUO vilivyokwishajengwa na vinavyotoa HUDUMA za AFYA ni:
*Murangi
*Mugango
*Bugwema

**KITUO KIPYA CHA AFYA CHA MAKOJO**
Kata ya MAKOJO yenye Vijiji 3 (Chimati, Chitare na Makojo) IMEAMUA kuongeza KASI ya ujenzi wa Kituo cha Afya ili kukikamilisha haraka iwezekanavyo.

Kata hii imepewa SHILINGI MILIONI 250 (Tsh 250m) kwa ajili ya ujenzi wa KITUO cha AFYA cha Kata yao. Fedha hizi ni RUZUKA ya SERIKALI yetu.

WANAVIJIJI wanachangia NGUVUKAZI zao kwa kuchimba misingi ya majengo, kusomba mawe, kokoto, mchanga na maji ya ujenzi.

WANANCHI na VIONGOZI wa Kata ya Makojo wanatoa shukrani nyingi sana kwa SERIKALI yetu inayoongozwa kwa umahiri mkubwa na RAIS wetu, Mhe Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN.

VIONGOZI wa Vitongoji wanahamasisha ushiriki wa Vitongoji vyao kwenye utekelezaji wa Mradi huu.

DIWANI wa Viti Maalum, Mhe Tabu Maregesi Machumu anasimamia ujenzi huu kwa ufanisi na mafanikio makubwa – tunampongeza sana!

MABOMA 2 tayari yanakaribia kuezekwa:
*OPD
*MAABARA

Ujenzi wa miundombinu mingine ya Kituo hiki, k.m. WODI ya Mama & Mtoto, unaendelea kwa kasi na ari mpya.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# FEDHA ZA TOZO KISIWANI RUKUBA

Posted on March 8, 2022



*Msingi wa Wodi ya Mama & Mtoto (Fedha za Tozo)*

WAKAZI na VIONGOZI wa Kisiwa cha Rukuba, Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kuishukuru SERIKALI na RAIS wetu, Mhe Dkt. SAMIA SULUHU HASSAN kwa kuwapatia SHILINGI MILIONI 250 za ujenzi wa KITUO cha AFYA cha Kisiwani humo.

FEDHA hizi ni za TOZO ya miamala ya simu.

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo anafuatilia kwa karibu sana ujenzi unaoendelea Kisiwani humo na kwingineko Jimboni, na hadi kufikia leo (Jumamosi, 5.3.2022) maendeleo ya ujenzi Kisiwani Rukuba ni kama ifuatavyo:

*MAABARA – Msingi wa Jengo lake umekamilishwa leo.

*WODI YA MAMA & MTOTO – Msingi wa Jengo unajengwa na utakamilishwa wiki ijayo. Picha hiyo hapo juu ya ukurasa huu.

## JENGO LILOJENGWA KWA NGUVU ZA WANA-RUKUBA & MBUNGE WA JIMBO

Hapo awali, Wakazi wa Kisiwani Rukuba (Wana-Rukuba) walianza ujenzi wa MIUNDOMBINU mipya ya kuboresha na kupanua Huduma za Afya zitolewazo na Zahanati ya Kisiwa hicho.

JENGO lilofikishwa kwenye renta litakamilishwa na matumizi yake yataelekezwa na Wataalamu wa Afya



*Boma linalojengwa kwa nguvu za Wana-Rukuba na Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo*

PICHA hapa chini inaonesha Jengo la Zahanati ya Kisiwa cha Rukuba (bati za rangi za bluu na kijani) – hii Zahanati inapanuliwa iwe Kituo cha Afya cha Kisiwa cha Rukuba.



*Jengo la Zahanati ya Kisiwa cha Rukuba*

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## FEDHA ZA UVIKO 19 (IMF): KISIWA CHA RUKUBA CHAKUBALI KUCHANGIA NGUVUKAZI KWENYE UJENZI WA KITUO CHAO CHA AFYA

Posted on January 9, 2022



*WAKAZI wa KISIWA cha RUKUBA wakisomba MCHANGA kwa ajili ya ujenzi wa MIUNDOMBINU ya KITUO chao cha AFYA.*

KISIWA cha RUKUBA kimepokea SHILINGI MILIONI 250 kwa ajili ya ujenzi wa KITUO cha AFYA Kisiwani humo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji/Kisiwa hicho, Ndugu Japhari Ibrahim Kibasa, kwa niaba ya WANA-RUKUBA, anatoa SHUKRANI nyingi sana kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa KUKIKUMBUKA KISIWA CHAO ambacho sasa kitakuwa na HUDUMA nzuri za Afya.

"Safari za MITUMBWI za mchana na usiku za kupeleka wagonjwa mahututi na wajawazito Musoma Mjini, sasa hazitakuwepo tena," amesema Kiongozi huyo.

Kisiwa cha Rukuba ni moja kati ya Vijiji 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini. Kisiwa hiki kiko Kata ya Etaro.

Leo, Ijumaa, tarehe 7.1.2022, WAKAZI wa Kisiwani humo wameanza kusomba mchanga wa ujenzi wa:
*Jengo la Maabara

*Wodi ya Mama&Mtoto
*Kichomea Taka (incinerator)

KISIWA cha RUKUBA kinang'ara sana kimaendeleo. Ndani ya MIAKA 6, Kisiwa cha Rukuba kimekamilisha yafuatayo:

**(1) SHULE YA MSINGI:**
*Vyumba vya Madarasa vipo vya kutosha na ziada ya chumba kimoja

**(2) MAKTABA YA SHULE YA MSINGI:**
*Wakazi wa Kisiwani humo walishirikiana na PCI Tanzania na Mbunge wao Prof Sospeter Muhongo kujenga MAKTABA na kuweka VITABU vya kutosha.

**(3) NYUMBA ZA WALIMU:**
*Mdau wa Maendeleo Kisiwani humo alishirikiana na Wakazi wa Kisiwa hicho kujenga nyumba za Walimu. Kila Mwalimu amepewa nyumba ya shule, na ipo moja ya ziada.

(**4) UMEME JUA (solar):**
*Mradi umeanza kutekelezwa wa utumiaji wa "solar". Zahanati inatumia "solar"

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## WANAVIJIJI WANAJENGA ZAHANATI MPYA 15 KWA AJILI YA UBORESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on October 12, 2021




*UJENZI unaondelea kwenye baadhi ya ZAHANATI, VITUO vya AFYA vya Musoma Vijijini.*

WANAVIJIJI wa JIMBO la MUSOMA VIJIJINI wamekuwa na mwamuko mkubwa wa KUJITOLEA kuanzisha na KUTEKELEZA MIRADI ya MAENDELEO yao kwenye Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Uvuvi, Ufugaji, Utamaduni na Michezo.

SERIKALI inatoa MICHANGO ya FEDHA kwenye utekelezaji wa baadhi ya Miradi hiyo ya Maendeleo.

**CHANJO DHIDI YA UVIKO-19**

Kesho, JUMATATU, tarehe 9.8.2021 kuna uzinduzi wa CHANJO ya COVID-19 kwenye Viwanja vya S/M KWIBARA, karibu na Makao Makuu ya Muda ya Halmashauri yetu.

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo ameishachanjwa (J&J jab) na Wasaidizi wake wote 5 watachanjwa.

**CHANJO HII NI SALAMA, SISI SOTE TWENDE TUKACHANJWE**

JIMBO hili lina KATA 21 zenye VIJIJI 68 na VITONGOJI 374
VITUO 28 VYA CHANJO YA UVIKO MUSOMA VIJIJINI viko vijijini:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bugoji | 2. Bugunda | 3. Bwasi |
| 4. Kiemba | 5. Kiriba | 6. Kome |
| 7. Kurugee | 8. Mugango | 9. Murangi |
| 10. Mwiringo | 11. Nyakatende | 12. Nyambono |
| 13. Rukuba (Kisiwa) | 14. Seka | 15. Suguti |
| 16. Tegeruka | 17. Wanyere | 18. Bwai Kwitururu |
| 19. Rusoli | 20. Bukima | 21. Busungu |
| 22. Chitare | 23. Etaro | 24. Kigera Etuma |
| 25. Kwikuba | 26. Masinono | 27. Nyegina |
| 28. Musoma dc hosp (kitongoji cha Kwikonero) | | |

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea KUJITOKEZA kupata CHANJO ya UVIKO. Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo alishachanjwa.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI MIPYA KWENYE SEKTA YA AFYA NDANI YA JIMBO LETU**

UJENZI wa:
*Zahanati 15
*Wodi 3 za Mama & Mtoto (Zahanati za Kisiwani Rukuba, Bukima & Nyegina)
*Vituo 2 vya Afya (Bugwema & Makojo: kwa mchango mkubwa Serikali)
*Hospital ya Wilaya inayojengwa na Serikali (haijakamilika: kila Kijiji kinachangia Tsh milioni 2)

**HUDUMA ZA AFYA ZILIZOPO**

*Zahanati 23 za Serikali
*Zahanati 4 za Binafsi
*Vituo vya Afya 3 (Murangi, Mugango & Bugwema)
*Magari 5 ya Wagonjwa (Ambulances 5: zilitolewa na Mbunge wa Jimbo)

**ZAHANATI MPYA 15 ZINAZOJENGWA NA WANAVIJIJI**

1. Buira, Kijiji cha Buira, Kata ya Bukumi
2. Busekera, Kijiji cha Busekera, Kata ya Bukumi
3. Burungu, Kijiji cha Bukumi Kata, Bukumi
4. Butata, Kijiji cha Butata Kata, Bukima
5. Bwai Kwitururu, Kijiji cha Bwai Kwitururu, Kata ya Kiriba
6. Chimati, Kijiji cha Chimati, Kata ya Makojo
7. Chirorwe, Kijiji cha Chirorwe, Kata ya Suguti
8. Kakisheri, Kijiji cha Kakisheri, Kata ya Nyakatende
9. Kurukerege, Kijiji cha Kurukerege, Kata ya Nyegina
10. Kurwaki, Kijiji cha Kurwaki, Kata ya Mugango
11. Maneke, Kijiji cha Maneke, Kata ya Busambara
12. Mkirira, Kijiji cha Mkirira, Kata ya Nyegina
13. Mmahare, Kijiji cha Mmahare, Kata ya Etaro
14. Nyabaengere, Kijiji cha Nyabaengere, Kata ya Musanja
15. Nyasaungu, Kijiji cha Nyasaungu, Kata ya Ifulifu

*Baadhi ya Zahanati hizo zimepokea MICHANGO ya FEDHA kutoka SERIKALI KUU

*Wanavijiji na Viongozi wao (Mbunge wa Jimbo & Madiwani), na baadhi ya Wazaliwa wa Musoma Vijijini) ndio WACHANGIAJI WAKUU wa ujenzi huo.

*Halmashauri yetu (Musoma DC) inashauriwa nayo ianze kuchangia ujenzi wa Zahanati hizo.

**AMBULACE 5 ZA MUSOMA VIJIJINI**

Katika kuboresha Huduma za Afya Jimboni mwao, Mbunge wa Jimbo, Profesa Sospeter Muhongo, alitoa magari matano ya wagonjwa ambayo kwa sasa yamechoka baada ya kutumika kwa muda mrefu, Ambulance hizo zilipelekwa:

- Kituo cha Afya Murangi, Kata ya Murangi
- Kituo cha Afya Mugango, Kata ya Mugango
- Zahanati ya Kurugee, Kijiji cha Bukumi, Kata ya Bukumi
- Zahanati ya Masinono, Kijiji cha Masinono, Kata ya Bugwema
- Zahanati ya Nyakatende, Kijiji cha Kabegi, Kata ya Ifulifu

**OMBI KUTOKA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI**

Wananchi na Viongozi wa Jimbo hili wanaomba MICHANGO ya FEDHA (zikiwemo Fedha za IMF) wakamilishe UJENZI wa MIUNDOMBINU ya AFYA ya Jimboni mwao.

Vilevile, WANAVIJIJI wanaomba MAGARI 2 ya WAGONJWA (2 Ambulances) kwa kuzingatia ukubwa wa Jimbo hili.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# SERIKALI YATOA TSH MILIONI 50 KUUNGA MKONO JUHUDI ZA WANAKIJIJI KWENYE UJENZI WA ZAHANATI YA KIJIJI CHAO

Posted on September 19, 2021



*Hatua zilizofikiwa kwenye ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mkirira, Kata ya Nyegina*

Jimbo la Musoma Vijijini lenye Kata 21 zenye jumla ya Vijiji 68 lina Huduma za Afya zifuatazo:
*Hospitali ya Wilaya ya Serikali, ujenzi unaendelea kwenye Kitongoji cha Kwikonero, Kijijini Suguti.
*Vituo Vya Afya 3 vya Serikali vinatoa Huduma za Afya. Vituo hivi ni:

- Murangi
- Mugango
- Bugwema (Ujenzi wa upanuzi wa Zahanati ya Masinono kuwa Kituo cha Afya unakamilishwa)

Zahanati ya Makojo imepewa fedha (Tsh 250m) na Serikali kupanuliwa iwe Kituo cha Afya, hivyo kitakuwa Kituo cha Afya cha nne (4) Jimboni mwetu.

*Zahanati 23 za Serikali zinatoa Huduma za Afya
*Zahanati za Binafsi zipo 4, nazo pia zinatoa Huduma za Afya.
*Zahanati Mpya 15 zinajengwa na Wanavijiji. Serikali imeanza kuchangia ujenzi wa baadhi ya Zahanati hizi.

**UJENZI WA ZAHANATI YA KIJIJI CHA MKIRIRA**

Kijiji cha Mkirira kiko Kata ya Nyegina, inayoundwa na Vijiji 3 (Kurukerege, Mkirira na Nyegina). Kijiji hiki kina jumla ya Wakazi 5,696.

Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mkirira ulianza Mwaka 2016. Ujenzi huu unaendeshwa kwa kutumia MICHANGO ya WANAKIJIJI, SERIKALI KUU (TAMISEMI), MBUNGE WA JIMBO, na WADAU WENGINE wa MAENDELEO.

**WACHANGIAJI WA UJENZI:**

**WANAKIJIJI:**

Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Mkirira, Ndugu Sabina Chacha amesema kuwa hadi hapo ujenzi ulipofikia nguvu za WANANCHI ni za thamani ya Tsh. Milioni 16. Hii inajumuisha nguvukazi za kusomba maji, mchanga, mawe, kokoto na michango ya fedha taslimu.

Wanakijiji walikubaliana kuchangia Tsh. 15,850/= kwa kila mkazi wa Kijijini hapo na mwenye umri wa kuanzia miaka 18.

**SERIKALI KUU:**

Serikali Kuu (TAMISEMI) imechangia Tsh. Milioni 50. Hii ni kwa ajili ya ukamilishaji (finishing) wa Zahanati hii ya Mkirira. SHUKRANI NYINGI SANA kwa SERIKALI yetu.

**MBUNGE WA JIMBO:**

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo amechangia SARUJI MIFUKO 200 kwenye ujenzi wa Zahanati hii.

**MICHANGO YA WADAU WENGINE WA MAENDELEO**

*Mhe Amina Makilagi
Saruji Mifuko 180

*Benki ya NMB
Mabati 180

*Nyanza Road Works Ltd
(i) Kokoto tripu 6
(ii) Saruji Mifuko 50

*Mhe Majira Mchele (Diwani wa Kata ya Nyegina) amechangia Tsh 700,000/=

*Kikundi cha WAZALIWA wa Kijiji cha Mkirira wamechangia:
(i) Kokoto tripu 3
(ii) Saruji Mifuko 30
(iii) Nondo 4

MIUNDOMBINU inayojengwa kwenye Zahanati ya Kijiji cha Mkirira ni:
* Opd
* Chumba cha Daktari
* Maabara
* Wodi la Mama & Mtoto
* Wodi la Wagonjwa wengine
* Chumba cha Wajawazito
* Chumba cha Uzazi wa Mpango
* Chumba cha dawa
* Chumba cha chanjo

**LENGO WALIOJIWEKEA WANAKIJIJI:**
Kwa kuwa wakazi wa Kijiji cha Mkirira wamekuwa wakitembea umbali mrefu wa kilomita 8-10 kwenda kupata Huduma za Afya kwenye Zahanati ya Kijiji jirani cha Nyegina, WANAKIJIJI hao wameamua kukamilisha ujenzi wa Zahanati yao ifikapo Novemba 2021. Hayo yameelezwa na Ndugu Paschal Maerere, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mkirira.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI
# WA
# MIRADI
# YA
# KILIMO, UVUVI
# NA
# UFUGAJI

**(30 Juni 2022 – 1 Julai 2021)**

# KAMPENI KABAMBE YA UPANDAJI MICHE YA MITI NA MATUNDA WAANZA MUSOMA VIJIJINI

Posted on May 21, 2022



*Mbunge wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo akigawa MICHE 10,000 kwa Wanafunzi na Wanavijiji wa Jimboni mwetu*

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo ANASHIRIKIANA na VI Agroforestry Project ya AIC (African Inland Church) kupanda miche ya MITI na MATUNDA vijijini mwetu, zikiwemo shule zetu zote na Madhehebu ya Dini zote. Wakulima binafsi nao wanapewa miche ya miti na matunda.

Miche ya miti na matunda inatolewa bure na iwapo inapaswa kununuliwa (k.m. miche ya mivule), Mbunge huyo anainunua na kuigawa bure.

Jumatano, tarehe 18.5.2022, Mbunge huyo aliambatana na Mtaalamu wa Misitu, Ndugu Jacob Malima wa VI Agroforestry Project KUGAWA MICHE 10,000 (miche elfu kumi) kwenye vijiji vya kando kando mwa Ziwa Victoria (Vijiji vya Kurwaki, Kiriba, Bwai Kumsoma), kikiwepo Kisiwa cha Rukuba (miche 4,500)

**MVUA ZA VULI ZA MWEZI OKTOBA**

Mipango inawekwa na DC (Dr Khalifany Haule) na DED (Ndugu Msongela Palela) wetu kwenye UPANDAJI mkubwa wa MITI na MATUNDA ndani ya vijiji vyetu 68 ikiwemo Milima yetu (k.m. Nyabherango na Mtiro) ambayo kwa sasa ni vipara vitupu.

Malengo yetu ni kupanda MICHE 100,000 (miche laki moja) wakati wa mvua za vuli za Oktoba 2022.

Usisahau kutembelea TOVUTI ya Jimbo letu ambayo ni: www.musomavijijini.or.tz

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KILIMO CHA UMWAGILIAJI NA UTUMIAJI WA JEMBE LA KUKOKOTWA NA NG'OMBE (PLAU) VYAONGEZA MAVUNO YA KILIMO MUSOMA VIJIJINI

Posted on August 10, 2021



*Wanachama wa KIKUNDI cha ANGAZA wakiandaa Shamba lao la matikiti Kijijini Bukumi*

## SALAMU ZA HERI ZA NANE NANE KWA WAKULIMA WA MUSOMA VIJIJINI

SHEREHE za NANE NANE hazikufanyika Mwaka huu kuepuka MADHARA ya KORONA. Tarehe nyingine itapangwa kwa ajili ya Mashindano yetu ya kila Mwaka ya Nane Nane – Ngoma za Asili & Kwaya.

## UBORESHAJI WA KILIMO JIMBONI MWETU

JIMBO la Musoma Vijijini linafanya yafuatayo kuboresha KILIMO cha WAKULIMA wake:

*WAKULIMA wanashawishiwa waunde VIKUNDI vya KILIMO ili kurahisisha upatikanaji ya MAHITAJI yao ya Kilimo

*KILIMO cha UMWAGILIAJI kinawekewa mkazo sana, kwani hatuko mbali na Ziwa Victoria.

*ZAO JIPYA la ALIZETI linastawi vizuri kwenye udongo wetu.

*PLAU, Jembe la kukokotwa na ng'ombe linagawiwa bure kwenye Vikundi vya Kilimo. Hizi ni jitihada za kupunguza utumiaji wa JEMBE la MKONO.

**KIKUNDI CHA ANGAZA CHA KIJIJI CHA BURAGA**

KIJIJI cha BURAGA ni kimoja kati ya Vijiji 4 vya KATA ya BUKUMI. Vijiji vingine ni Buira, Bukumi na Busekera.

KIKUNDI cha ANGAZA chenye Makazi yake Kijijini Buraga, kilianzishwa Mwaka 2015 na kinafanya shughuli zake za KILIMO kwenye Kijiji cha BUKUMI.

MWENYEKITI wa Kikundi hiki, Ndugu Pius Bwire ameeleza kwamba KIKUNDI chao:

*Kina Wanachama 11

*Wanajishughulisha na kilimo cha BUSTANI za matikiti, matango, nyanya na maboga aina ya batanati

*Baada ya kupata nyenzo bora za kilimo, watapanua mashamba yao ili kupanua KILIMO cha MAZAO ya BIASHARA yakiwemo ya alizeti, mahindi na mihogo.

AFISA KILIMO wa Kata ya Bukumi, Ndugu Alex Mihambo amekuwa akitembelea KIKUNDI hicho na vingine kwa ajili ya kutoa mafunzo, ushauri na maelekezo ya kitaalamu.

AFISA huyo wa Kilimo amesema MAFANIKIO ya KIKUNDI cha ANGAZA yamehamasisha na kutoa mvuto mkubwa kwa WAKULIMA wa KATA hiyo kujiunga kwenye VIKUNDI vya KILIMO na kuanza KILIMO cha BUSTANI chenye kutumia MAJI ya Ziwa Victoria kwa UMWAGILIAJI.

Wakulima wameanza kuongeza mavuno ya mahindi kutoka magunia 4-5 kwa ekari hadi 8-10 kwa ekari.

**MCHANGO WA MBUNGE WA JIMBO KWENYE UBORESHAJI WA KILIMO VIJIJINI MWAO**

MBUNGE wa Jimbo akishirikiana na SERIKALI anafanya/amefanya yafuatayo:

*Kugawa bure MBEGU za ALIZETI. Mbunge aligawa bure TANI 9.85 za mbegu za Alizeti, na WIZARA ya KILIMO ilichangia TANI 10 za mbegu hiyo.

*MBUNGE aligawa bure mbegu za mihogo, mtama na ufuta

*MBUNGE anayo Programu yake ya kugawa bure PLAU kwenye Vikundi vya Kilimo vya Vijiji vyote 68 vya Jimbo hili.

**MICHANGO YA MBUNGE WA JIMBO KWENYE KATA YA BUKUMI**

*Kugawa MBEGU za alizeti, mihogo na mtama kwenye Vijiji vyote 4 vya Kata hii

*Kugawa PLAU 5 kwenye Vikundi vya Kilimo vya Kata ya Bukumi ambavyo ni: Amani Group, Mshikamano, Umoja ni Nguvu, Nyabigoma na Majita Group

*Kutoa MASHINE ya UMWAGILIAJI kwa Kikundi cha Angaza kutoka kwenye FEDHA za MFUKO wa JIMBO

KARIBUNI TUBORESHE KILIMO VIJIJINI MWETU – Tununulie ndugu zetu PLAU waachane na Jembe la Mkono. VIKUNDI vingi vinaomba MASHINE za UMWAGILIAJI

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# KILIMO CHA MIHOGO CHAENDELEA KUBORESHWA MUSOMA VIJIJINI

Posted on July 5, 2021



*WANACHAMA wa Kikundi cha KILIMO cha TUMEJITAMBUA wakiwa kwenye kazi za UOTESHAJI wa MITI na kwenye mashamba yao ya MIHOGO. Hapo ni Kijijini Bwenda, Kata ya Rusoli*

MAZAO MAKUU ya CHAKULA yalimwayo Jimboni mwetu ni: mihogo, mahindi, viazi vitamu, mtama, mpunga, maharage na kunde.

MBOGAMBOGA (k.m., mchicha, kabechi, nyanya, vitunguu) na MATUNDA (matikiti, maembe na machungwa) navyo vinalimwa Vijijini mwetu.

KIKUNDI cha KILIMO kiitwacho TUMEJITAMBUA cha Kijijini Bwenda, Kata ya Rusoli kinajishughulisha na UBORESHAJI wa KILIMO cha MIHOGO.

KIKUNDI hiki kilianzishwa Mwaka 2018 na kina WANACHAMA 31.
Mbali ya kilimo cha MIHOGO, KIKUNDI hiki nacho kiko kwenye Kilimo cha mahindi, maharage, viazi lishe, uoteshaji wa miti, na WANACHAMA wake wanakopeshana fedha.

**UBORESHAJI WA KILIMO CHA MIHOGO**

KIKUNDI cha TUMEJITAMBUA kimeanzisha SHAMBA DARASA la kilimo cha MIHOGO ambalo limekuwa kivutio kikubwa kwa wakulima wa eneo hilo na vijiji vingine.

**LENGO KUU la KIKUNDI hiki cha KILIMO ni:**

*Kufanya biashara ya mazao ya chakula, ikiwemo biashara ya VIJITI vya MIHOGO

*Kuanzisha KIWANDA kitakachozalisha bidhaa zitokanzo na ZAO LA la MIHOGO kama vile, unga, wanga na biskuti.

KATIBU wa KIKUNDI hicho, Ndugu Festo Obed ameeleza jinsi KIKUNDI hicho kilivyopata mafunzo ya uzalishaji wa MBEGU za MIHOGO kutoka Shirika la MEDA (Mennonite Economic Development Associates)

KIKUNDI hicho kimelima aina mbili za mbegu za mihogo, yaani wamepanda Vijiti 4,000 vya mbegu ya TARICAS 4 (Tz 130) na wanategemea kuvuna Vijiti 48,000 ya aina hii ya mbegu.

Vilevile, kwa mbegu ya pili ya MKURANGA 1, wamepanda Vijiti 7,000 na wanategemea kuvuna Vijiti 42,000.

MBEGU zote hizi zinachukua muda wa MIEZI 9 kupata mavuno mazuri ya MIHOGO.

Baada ya Mbegu mbili hizo kutoa MAFANIKIO mazuri, Mtaalam wa MEDA, Ndugu Isaack Musa ameshawishi KIKUNDI hicho kuchukua MBEGU nyingine ambazo nazo zinastahimili magonjwa ya mimea na athari za tabianchi.

MBEGU nyingine za MIHOGO zilizotolewa na MEDA ni aina ya Mkuranga, Mkumba, Kizimbani, Taricas 2 (F10) na Kiroba.

**MIKOPO NA MISAADA ILIYOTOLEWA KWA KIKUNDI CHA KILIMO CHA TUMEJITAMBUA**

Kikundi cha KILIMO cha TUMEJITAMBUA kinatoa shukrani nyingi kwa wafuataao:
*MEDA kwa kuwapatia MBEGU mbalimbali za MIHOGO.

*JAMII IMPACT kwa kuwapatia Mkopo wa SHILINGI MILIONI 5 (awamu ya kwanza) na SHILINGI MILIONI 10 (awamu ya pili), na hivi karibuni watapokea mkopo mwingine.

*PCI Tanzania kwa kuwapatia mbegu za mahindi, maharage, alizeti na magunia ya kuhifadhia chakula

*SHIMAKIUMU kwa kuwapatia mbegu za mahindi, dawa za mimea na miroba vya kupandia miche

*MBUNGE wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Muhongo kwa kuwapatia mbegu za mihogo, mtama na alizeti

MBUNGE wa Jimbo, Prof Sospeter Muhongo alishagawa bure mbegu (Vijiti) aina ya Mkombozi kwa wakulima wa Jimboni mwetu kama ifuatavyo:
*MSIMU wa Kilimo wa Mwaka 2016/2017:
Magunia 446

*MSIMU wa Kilimo wa Mwaka 2017/2018:
Magunia 350

**KARIBUNI KIJIJINI BWENDA (Kata ya Rusoli) MNUNUE VIJITI VYA MBEGU ZA MIHOGO**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI

## (30 Juni 2022 – 1 Julai 2021)

**Tarehe 6.2.2022**

- Mradi wa thamani ya Tsh. Bilioni 70.5 ulizinduliwa Kijijini Kwibara, Kata ya Mugano na Mhe Rais Dkt Samia Suluhu Hassan
- Huu ni Mradi wa Bomba la Maji la Mugango-Kiabakari-Butiama

# MRADI WA MAJI WA TSH. BILIONI 70.5 – UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI

Posted on February 11, 2022



*Mhe RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, MHE DKT SAMIA SULUHU HASSAN aliweka JIWE la MSINGI kwenye Mradi wa ujenzi wa BOMBA la MAJI la Mugango-Kiabakari-Butiama utakaogarimu Tsh BILIONI 70.5*

Jumapili, tarehe 6.2.2022, RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan aliweka JIWE la MSINGI kwenye Mradi wa ujenzi wa BOMBA la MAJI la Mugango-Kiabakari-Butiama utakaogharimu Tsh BILIONI 70.5 – haya ni MAJI ya kutoka Ziwa Victoria.

TUKIO hilo lilifanyika ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini, Kijijini KWIBARA, MUGANGO

VIKUNDI vya KWAYA na NGOMA za ASILI vya Jimboni mwetu vilitoa burudani wakati wa sherehe hizo muhimu sana zilizofanyika Jimboni mwetu.

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAJI YA ZIWA VICTORIA: VIJIJI VINGINE VITATU VYAPATA MAJI YA BOMBA

Posted on January 2, 2022




*Vijiji vya Bukumi, Buraga na Busekera vimeanza kutumia Maji SAFI & SALAMA*

MWAKA MPYA na CHANZO KIPYA CHA MAJI – Vijiji vya Bukumi, Buraga na Busekera vimeanza kutumia Maji SAFI & SALAMA baada ya Mradi wao wa Maji kukamilika.

RUWASA inaendelea kutekeleza kwa mafanikio makubwa MIRADI ya USAMBAZAJI MAJI vijijini mwetu.

WANAVIJIJI na VIONGOZI wao wanatoa SHUKRANI zao za dhati kwa SERIKALI yao.

**MAJI NI UHAI**
**MAJI NI UCHUMI**
**MAJI NI MAENDELEO**

Taarifa kutoka:
*Ofisi ya RUWASA, Musoma DC

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# RUWASA YAENDELEA KUSIFIWA MUSOMA VIJIJINI

Posted on December 28, 2021




*Wanavijiji wa KASTAMU, BUANGA na BUTATA sasa wanao uhakika wa kupata MAJI SAFI na SALAMA majumbani mwao*

Maji safi na salama ya BOMBA kutoka Ziwa Victoria yaanza kutumika ndani ya VIJIJI 3 vya KASTAMU, BUANGA na BUTATA

SHUKRANI nyingi sana zimetolewa kwa Serikali yetu kwa kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huu.

Taarifa kutoka:
*Ofisi ya RUWASA, Musoma DC

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# FEDHA ZA COVID-19 KUPELEKA MAJI KWENYE VIJIJI VINGINE VIWILI VYA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on November 7, 2021



*Ujenzi na uwekaji wa baadhi ya MIUNDOMBINU ya Bomba la Maji la Mugango-Kiabakari-Mugango*

WANANCHI na VIONGOZI wa Jimbo la Musoma Vijijini wanaendelea kutoa SHUKRANI NYINGI kwa SERIKALI yao inayoongozwa na MHE DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa KUWAPATIA FEDHA ZA COVID-19 kwa ajili ya usambazaji maji ya bomba vijijini mwao.

*Tsh MILIONI 500 zimetolewa kwa ajili ya kusambaza maji ya bomba kwenye Vijiji 3 vya: KANDEREMA, BUGOJI na KABURABURA. Mradi huu wa maji kutoka Ziwa Victoria tayari unatekelezwa, na chanzo cha maji kiko Kijijini Suguti, Kata ya Suguti. Mradi huu unatekelezwa wa RUWASA, Musoma Vijijini

*Tsh MILIONI 300 zitatumika kusambaza maji kwenye Vijiji 2 vya: KURWAKI (Kata ya Mugango) na NYASAUNGU (Kata ya Ifulifu). Huu nao ni Mradi wa maji ya Ziwa Victoria na chanzo chake kiko Kijijini Kwibara, Kata ya Mugango

Mradi huu wa Vijiji 2 utakuwa sehemu ya Mradi Mkuu wa Bomba la Maji la Mugango-Kiabakari-Butiama.

TAARIFA ya utekelezaji wa Mradi wa Bomba la Maji la Mugango-Kiabakari- Butiama, utakaogharimu Tsh BILIONI 70, itatolewa hivi karibuni.

Taarifa kutoka:
*Ofisi ya RUWASA, Musoma DC
*Ofisi ya Mradi wa Mugango-Kiabakari-Butiama

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# FEDHA ZA COVID-19 KUPELEKA MAJI YA BOMBA KWENYE VIJIJI VITATU (3)

Posted on October 24, 2021



*Tenki la Maji (Lita 200,000 – lenye ngazi pichani) ya Vijiji vya Saragana, Nyambono na Mikuyu lililojengwa Mlimani Nyabherango, Kijijini Nyambono*

JIMBO la Musoma Vijijini limepata Tsh MILIONI 500 za COVID-19 kwa ajili ya kusambaza maji vijijini mwetu.

MATUMIZI YA FEDHA hizo za COVID-19 ni kama ifuatavyo:

*Ujenzi wa TENKI la MAJI la mita za ujazo 200 (lita 200,000) Mlimani Nyabherango, Kijijini Nyambono.

*Usambazaji wa MABOMBA ya Maji kutoka kwenye TENKI hilo kwenda Vijiji vya KANDEREMA, BUGOJI na KABURABURA.

*Mlimani Nyabherango (Kijijini Nyambono) tayari lipo TENKI la MAJI (200 cu.m./lita 200,000) kwa ajili ya MAJI ya Vijiji vya SARAGANA, NYAMBONO na MIKUYU. Tenki hili limejengwa kwa kutumia Fedha za Bajeti za Mwaka 2019/2020

**CHANZO CHA MAJI YA BOMBA YA VIJIJI HIVI SITA (6)**
*Fedha za Bajeti ya Mwaka 2019/2020 na Mwaka 2020/2021 zimewezesha ujenzi wa MIUNDOMBINU ya kutumia Maji ya Ziwa Victoria kutoka kwenye chanzo kilichopo Kijijini Suguti.

*Maji ya kutoka Kijijini SUGUTI yanapelekwa hadi Kijijini CHIRORWE ambapo mabomba yametandazwa kupeleka maji Kijijini WANYERE na mengine kupeleka maji, kupitia Mlima Nyabherango, kwenda Vijijini SARAGANA, NYAMBONO na MIKIYU.

**OMBI KWA WANAVIJIJI**
*Wakazi wa vijiji vyote 6 wanaombwa kurahisisha upatikanaji wa maeneo ya kutandaza mabomba ya kusafirisha maji yatakayokuwa kwenye MATENKI 2 Mlimani Nyabherango.

*Wanavijiji wanaombwa kuchangia NGUVUKAZI kuchimba mitaro ya kutandaza mabomba ya maji – tujitolee na tuchangie upatikanaji wa MAJI ya BOMBA Vijijini mwetu.

**KUKAMILIKA KWA MRADI HUU**
*Imepangwa kwamba, ifikapo tarehe 30 Disemba 2021, MAJI ya BOMBA yaanze kutumika ndani ya VIJIJI 6 vya: MIKUYU, NYAMBONO, SARAGANA, KANDEREMA, BUGOJI na KABURABURA

**SHUKRANI:**
*Shukrani za dhati zinatolewa na Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini kwenda kwa SERIKALI YETU, na haswa kwa MHE RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, MHE DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, kwa kufanikisha upatikanaji wa FEDHA za COVID-19 na nyingine kwa manufaa ya TAIFA LETU.

Taarifa kutoka:
*Ofisi ya RUWASA, Musoma DC

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MAELEZO YA UTEKELEZAJI
# WA
# MIRADI
# YA
# UJENZI WA BARABARA

**(30 Juni 2022 – 1 Julai 2021)**

# BARABARA ZINAZOJENGWA NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on February 23, 2022



*A – FEDHA ZA BAJETI YA MAENDELEO*
*(ROAD FUND DEVELOPMENT BUDGET) 2021/2022*

1. Mkirira – Kwangwa Hospital (Gharama: Tsh Milioni 350). Limekamilika kwa 90%

2. Bukima-Bulinga- Bwasi (Gharama: Tsh Milioni 300). Ujenzi umekamilika

## B – FEDHA ZA JIMBO

Masinono – Kinyang'erere (Gharama: Tsh Milioni 500). Likiwemo Daraja la Jitirola na mengine mawili. Hatua za kumpata Mkandarasi zinakamilishwa

## C – FEDHA ZA TOZO

(Jumla: Tsh bilioni 2)

Barabara zinazojengwa na utekelezaji umeanza:
(1) Mmahare-Etaro-Nyasaungu
(2) Mugango-Bwai Kwitururu- Kwikuba
(3) Bwai Kwitururu- Bwai Kumsoma
(4) Maneke-Mayani- Kyawazaru
(5) Nyaminya-Kataryo- Kyawazaru
(6) Rwanga-Seka-Mikuyu
(7) Saragana- Nyambono- Chumwi
(8) Kaburabura-Masinono-Bugwema
(9) Bukima-Bulinga- Bwasi
(10) Busekera-Burungu
(11) Chitare-Kurugee-Buraga (Kivukoni)
(12) Kome – Buira
(13) Kigera Etuma-Ekungu
(14) Nyakatende-Kamguruki- Kigera Etuma
(15) Mkirira-Nyegina-Esira
(16) Kurukerege-Nyegina

TAARIFA kutoka:
*Ofisi ya TARURA (W), Musoma DC

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

## SERIKALI YAENDELEA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA BARABARA ZA MUSOMA VIJIJINI

Posted on August 13, 2021



*Kazi inaendelea Kijijini Bugunda kwenye ujenzi wa DARAJA la MTO NYAMWIFA.*

DARAJA la Mto Nyamwifa ni muhimu sana kwenye barabara inayounganisha Vijiji vya Bukima, Bulinga na Bwasi – yaani barabara hii inaunganisha KATA 3 zenye BIASHARA za mazao ya UVUVI na KILIMO.

MTENDAJI wa KATA ya Bwasi, Ndugu Mashaka Kagere ameeleza kuwa Daraja hilo liliharibika Mwaka 2018 na kupelekea shughuli za kijamii kuzorota sana. Magari ya kusafirisha SAMAKI kutoka Kome Beach yalishindwa kusafirisha bidhaa hiyo. Hata magari ya abiria yalisimama kufanya kazi huko.

MENEJA wa TARURA (W), Injinia Hussein Abbas ameeleza kuwa wamepata SHILINGI MILIONI 300 kutoka MFUKO wa BARABARA (ROAD FUND) kwa ajili ya MRADI wa DARAJA la Mto Nyamwifa na barabara za eneo hilo. FEDHA hizo zitatumika kwenye:

*ujenzi wa daraja

*ujenzi wa barabara ya km 5.0

*ujenzi wa kalavati 3

*uchimbaji wa mitaro na uwekaji wa kifusi sehemu korofi

MKANDARASI M/s Flow Services and Supplies Ltd ndiye anayetekeleza MRADI huu unaopaswa kukamilika kabla ya mvua za vuli kuanza kunyeesha (Oktoba 2021).

WANAVIJIJI wa Kata 3 (Bukima, Bulinga na Bwasi), WAFANYA BIASHARA na VIONGOZI mbalimbali wanaishukuru sana SERIKALI kwa kutoa FEDHA za kutatua TATIZO hili lilowasumbua tokea Mwaka 2018.

MBUNGE wa JIMBO, Profesa Sospeter Muhongo amekuwa akifuatilia kwa ukaribu sana MIRADI ya BARABARA zote za Musoma Vijijini.

MBUNGE huyo anaishukuru sana SERIKALI kwa kupitisha BAJETI ya SHILINGI BILIONI 2.85 kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa barabara za Musoma Vijijini kwa Mwaka huu wa Fedha (2021/2022).

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# TARURA WILAYA YA MUSOMA YAENDELEA KUKAMILISHA MIRADI YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Posted on July 16, 2021



*Daraja la Chuma lililojengwa juu ya Mto Suguti kwenye Barabara ya Wanyere-Suguti.*

## BARABARA YA WANYERE – KATARYO

## DARAJA LA CHUMA

Uwekaji wa Daraja la Chuma kwenye MTO SUGUTI utaboresha utumiaji wa BARABARA ya WANYERE – KATARYO.

Barabara hii ni muhimu sana kwa UCHUMI na HUDUMA za JAMII wa Kata za Tegeruka na Suguti, na kwa Jimbo letu kwa ujumla wake.
Baada ya ujenzi wa kuta imara (abutment walls) kukamilika, Daraja la Chuma tayari limekwa na barabara imeanza kutumika.

## BAJETI YA MWAKA 2021/2022

Bajeti ya SHILINGI BILIONI 2.85 itatumika kujenga na kukarabati barabara nyingi za Jimboni mwetu

**SHUKRANI:**
Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanatoa SHUKRANI nyingi sana kwa SERIKALI yetu kwa kutoa FEDHA za kujenga na kukarabati miundombinu ya BARABARA zetu za Vijijini – AHSANTE SANA!

Taarifa kutoka:
*Ofisi ya TARURA (W), Musoma DC

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MICHEZO NA UTAMADUNI

## (30 Juni 2022 – 1 Julai 2021)

## UIMARISHAJI WA UTAMADUNI NA MICHEZO NDANI YA JIMBO LA MUSOMA VIJIJINI

Posted on October 19, 2021



JIMBO la Musoma Vijijini lenye KATA 21 zenye VIJIJI 68 na VITONGOJI 374 limeamua kufufua na kuimarisha NGOMA za ASILI, KWAYA na MICHEZO ya aina mbalimbali chini ya ufadhili wa Mbunge wao wa Jimbo, Profesa Sospeter Muhongo.

USHAURI unaotolewa ni wa KILA KATA kuunda VIKUNDI au TIMU za kushindanishwa na KATA nyingine.

**MASHINDANO YA NGOMA ZA ASILI & KWAYA**

Sherehe za kila mwaka za NANE NANE zinatumika kumpata MSHINDI wa KWANZA hadi wa TATU kwenye mashindano ya Ngoma za Asili na Kwaya. Mbunge wa Jimbo ndiye mfadhili wa mashindano haya.

**MASHINDANO YA KUPIGA KASIA**
*Jimbo lina jumla ya Vikundi/Timu 18 za kupiga kasia

*Mashindano haya hufanyika kila mwisho wa mwaka kwa WAPIGA KASIA kushindana umbali wa kati ya mita 1,000 na 1,500 ndani ya Ziwa Victoria. Mfadhili wa mashindano haya ni Mbunge wetu wa Jimbo.

**MPIRA WA MIGUU JIMBONI MWETU**
*Jimbo lina TIMU 78 za Mpira wa Miguu. Mashindano ya Mchezo wa Mpira wa Miguu yanafanyika kwa nyakati tofauti Jimboni mwetu.

*Utaratibu unatengenezwa wa kupata TIMU ya MPIRA ya Jimbo letu ambayo itashiriki mashindano mbalimbali kwenye ngazi za Wilaya na Mkoa. Mbunge wa Jimbo alishagawa jezi na mipira kwa kila Kata, na hivi karibuni ataanza kugawa tena vifaa hivyo.

*Mbunge wa Jimbo alitoa mchango mkubwa kuipandisha TIMU ya BIASHARA ya Musoma Mjini kuingia LIGI KUU ya TAIFA.

*Vilevile, Mbunge wa Jimbo letu alikuwa mfadhili mkuu wa TIMU ya WASAGA (Kijiji cha Kasoma) iliyofanikiwa kuingia FAINALI YA LIGI DARAJA LA PILI ya Mkoa wa Mara.

**ORODHA NA IDADI YA VIKUNDI VYA NGOMA ZA ASILI ni** kama ifuatavyo:
*Jimbo lina Vikundi 27 vilivyogawanyika katika Makundi 5 kama ifuatavyo

(i) DOGOLI: Vikundi 4
(ii) GITAA: Kikundi 1
(iii) LIRANDI / LITUNGU: Vikundi 2
(iv) MBEGETE: Vikundi 3
(v) ZEZE: Vikundi 2

**IDADI YA KWAYA JIMBO MWETU**

*UIMBAJI ni kipaji cha pekee kwa Wana-Musoma Vijijini.

*Karibu kila Kijiji kina kwaya moja au zaidi. KWAYA kuu zinazotambulika ni 15.

**KARIBU UFURAHIE UTAMADUNI WA MUSOMA VIJIJINI – ILANI YA UCHAGUZI YA CCM INATEKELEZWA KWA VITENDO KWENYE MAENEO YOTE**

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

# MENGINEYO

## (30 Juni 2022 – 1 Julai 2021)

# KISIWA CHA RUKUBA KUSHIRIKI SHEREHE ZA CCM

Posted on February 5, 2022



*WAKAZI wa KISIWA cha RUKUBA wakishiriki katika kusomba SARUJI iliyonunuliwa Musoma Mjini na kusafirishwa hadi Kisiwani humo.*

Kesho, tarehe 5.2.2022 BOTI KUBWA 2 za kuchukua ABIRIA 80 zitaondoka Kisiwani Rukuba saa 10 alfajiri kupeleka WAWAKILISHI wao kwenye sherehe za CCM zitakazofanyika Musoma Mjini.

Kisiwa cha Rukuba ni moja ya vijiji 4 vya Kata ya Etaro ya Jimbo la Musoma Vijijini.

WAKAZI wa Kisiwa cha Rukuba wanaendelea kutoa SHUKRANI nyingi sana kwa RAIS wao, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia SHILINGI MILIONI 250 kujenga Kituo cha Afya kisiwani humo.

UJENZI umeanza na WAKAZI wa Kisiwani humo wamechangia ifuatavyo:

**(i) NGUVUKAZI:**
*wanasomba mawe, kokoto na maji ya ujenzi. Vilevile, wanachimba misingi ya majengo yote.

**(ii) SERIKALI YA KIJIJI/KISIWA**
*Imetumia mapato yake kununua vifaa vya kutumiwa kwenye ujenzi – pump 2 za kuvutia maji kutoka Ziwani na mipira yake, mapipa ya kutunzia maji ya ujenzi.

**FEDHA za UVIKO/IMF:**
Fedha ziko kwenye Akaunti ya Zahanati yao na tayari zimeanza kutumika kununua:

*Saruji Mifuko 599
*Nondo 210
*Mbao 32 za 1×8, 20 za 2×2
*Dawa ya kuua mchwa

TAARIFA hiyo hapo juu imetolewa na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji/Kisiwa, Ndugu Japhari Ibrahim Kabasa

Ofisi ya Mbunge
Jimbo la Musoma Vijijini
www.musomavijijini.or.tz

**HITIMISHO**

Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020-2025 unaenda vizuri Jimboni mwetu, na mafanikio yake yanaonekana na kuthaminiwa sana na wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini. Wanavijiji wanashirikiana na Serikali yao ya ngazi mbalimbali kuibua na kutekeleza miradi ya maendeleo inayokidhi mahitaji ya jamii zao.

Taarifa hii ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo letu ni ya mwaka mmoja wa fedha, yaani 1 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022. Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa Jimboni mwetu kwa kipindi hiki iliibuliwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025), ambamo ndimo tulitoa vipaumbele vyetu vitano vya maendeleo.

Miradi yetu ya maendeleo ni endelevu, kwani inaibuliwa kutoka kwenye vipaumbele vyetu vitano ambavyo navyo ni endelevu, na nyenzo kuu za utekelezaji wake nazo zinaendelea kuhitajika kwa ustawi wa jamii yetu.

Vipaumbele vyetu ni: (i) elimu, (ii) afya, (iii) kilimo, uvuvi na ufugaji, (iv) tabianchi na mazingira, na (v) michezo na utamaduni. Nyezo kuu zinazohitajika kwenye utekelezaji wa miradi ya vipaumbele vyetu ni maji, umeme, barabara, vyombo vya usafirishaji na mawasiliano, raslimali watu na taasisi za fedha na uchumi.

Ahadi zilizotolewa Jimboni mwetu na Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali yake, chini ya uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ziliendelea kutekelezwa ikiwemo ahadi ya ujenzi wa barabara la Musoma-Makojo-Busekera (km 92) kwa kiwango cha lami.

Ahadi za Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, zimetekelezwa na kuvuka malengo yaliyowekwa kwa mwaka huu mmoja (1 Julai 2021-30 Juni 2022).

Michango ya Mbunge huyu ni mingi na mikubwa kama inavyoainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini, anaendelea kushirikiana kwa ukaribu sana na wananchi, viongozi wa Chama (CCM) na wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye utekelezaji wenye mafanikio makubwa wa Ilani ya Uchaguzi (2020-2025) Jimboni mwao.

Vilevile, Mbunge huyu anaendelea kuchangia kwa kiasi kikubwa shughuli za Chama chetu (CCM) kwa ngazi zote, yaani, kuanzia Matawi, Kata, Wilaya (Musoma Vijijini), Mkoa (Mara) hadi Taifa (Tanzania).

## SHUKRANI

Wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini na viongozi wao wa ngazi za Vitongoji (374), Vijiji (68) na Kata (21), na Mbunge wao wa Jimbo, Prof Sospeter Mwijarubi Muhongo, wanatoa shukrani nyingi za dhati kwa Mwenyekiti wa CCM Taifa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa uwezeshaji na uongozi wake mzuri kwenye utekelezaji wa miradi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (1 Julai 2021 - 30 Juni 2022).

Rais wa Serikali ya Mapinduizi ya Zanzibar na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Mhe Dkt Hussein Ali Mwinyi anapewa shukrani nyingi kwa ushauri wake mzuri anaoutoa kwenye utekelezaji wa miradi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (1 Julai 2021-30 Juni 2022).

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Dkt Philip Isdor Mpango anapewa shukrani nyingi kwa ushauri na ufuatiliaji mzuri anaoufanya kwenye miradi ya maendeleo ya Jimboni mwetu.

Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Mhe Dkt Ali Mohamed Shein, Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Mhe Philipo Mangula, na Katibu Mkuu wa CCM Taifa, Ndg Daniel Chongolo nao wanapewa shukrani nyingi za dhati kwa usimamizi wao mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu (CCM) kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja (1Julai 2021-30Juni 2022).

Waziri Mkuu, Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa, na viongozi wengine wote wa ngazi mbalimbali za Serikali yetu wanapewa shukrani nyingi za uwezeshaji na ushirikiano wao kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo la Musoma Vijijini.

Kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja wa fedha (1 Julai 2021-30Julai 2022), utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Jimboni mwetu) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ulisimamiwa vizuri ki-Serikali na Wakuu wawili wa Mkoa wa Mara wa wakati huo ambao ni Mhe Ally Hapi na Mhe Meja Jenerali Suleiman Mzee.

Mkuu wa Wilaya yetu ya Musoma, Mhe Dkt Khalfany Boniface Haule anapongezwa na kupewa shukrani nyingi za dhati kwa uchapaji kazi wake mzuri wenye ufuatialiji na usimamiaji makini wa miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa Jimboni mwetu.

Shukrani nyingi pia zinatolewa kwa viongozi mbalimbali wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya zake kuanzia ngazi za Tawi, Kata, Wilaya hadi Mkoa (Mara). Baadhi yao ni Mlezi wa Mkoa ki-Chama, Ndugu Kheri James, M-NEC Mkoa, Ndugu Christopher Gachuma, Mwenyekiti wa Mkoa, Ndugu Samwel Kiboye, Katibu wa Mkoa, Ndugu Langaeli Akyoo. Wengine ni Mweyekiti wa CCM Wilaya ya Musoma Vijijini, Ndugu Nyabukika Bwire Nyabukika na Katibu wa Chama Wilaya, Ndugu Naboth Maiga Manyonyi na baadae Ndugu Noverty Bathromeo Kibaji.

Waheshimiwa Madiwani wote 28 wakiwemo wa Viti Maalumu, na wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma (Musoma DC) wanapewa shukrani za dhati kwa utimizaji wa wajibu wao kwenye utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu (CCM) ndani ya mwaka huu mmoja.

Shukrani nyingi inapewa RUWASA kwa kufufua miradi iliyokwama kwa miaka kadhaa, na kuanza utekelezaji wa miradi mipya ya usambazaji wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria, na uchimbaji wa visima virefu vya maji vijijini mwetu.

TARURA na TANROADS wanaendelea kuboresha barabara zetu ambazo zinapitika kwa urahisi kwa majira yote ya mwaka.

Vyanzo vya fedha na vifaa vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo vijijini mwetu iliyobuniwa kutoka kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2020-2025) ndani ya mwaka huu mmoja wa fedha (1 Julai 2021 - 30 Juni 2022) ni vingi vikiwemo: Serikali Kuu na miradi yake kama vile EQUIP, EP4R, Wadau wa Maendeleo (PCI Tanzania na BMZ Germany), Benki za NBC, NMB na CRDB.

Mbunge wa Jimbo ametoa michango mingi na mikubwa kuchangia utekelezaji wa miradi inayoelezwa ndani ya kitabu hiki. Wanavijiji wamechangia nguvukazi na fedha taslimu. Baadhi ya Wazaliwa wa Musoma Vijijini wametoa michango yao na majina yao yametajwa ndani ya kitabu hiki. Michango kutoka kwa Wadau wengine wa Maendeleo ya Jimboni mwetu imeainishwa ndani ya kitabu hiki.

Mbunge wa Jimbo anapenda kuwashukuru watu mbalimbali wenye fani mbalimbali anaofanya nao kazi za Jimbo la Musoma Vijijini. Orodha ni ndefu na kwa uwakilishi wao anamshukuru Mtendaji Mkuu (Webmaster) wa Tovuti ya Jimbo letu (www.musomavijijini.or.tz), Dkt Isack Kambira.

Wengine wanaopewa shukrani ni Waandishi wa Habari wakiwakilishwa na Ndugu Sadick Hunga, John Makali na Shomari Binda. Wafanyakazi wa Ofisi ya Mbunge wanapewa shukrani nyingi kwa kazi zao nzuri - hao ni Vaileth Peter, Fedson Masawa, Verediana Mgoma na Hamisa Gamba.

Shukrani za kipekee na za muhimu sana zinapewa WANANCHI wa Jimbo la Musoma Vijijini ambao kwa utashi wao wenyewe wameamua kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025. Miradi ya maendeleo inayotekelezwa

vijijini mwao inabuniwa, inachangiwa (nguvukazi na fedha taslimu), inatekelezwa na inatunzwa na wao wenyewe.

Vilevile, wananchi wa Jimbo la Musoma Vijijini wanashirikana vizuri sana na Chama cha Mapinduzi (CCM) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa manufaa makubwa ya ukuaji, uimarikaji wa uchumi na ustawi wa Jimbo letu la Musoma Vijijini.

Kitabu hiki kimetayarishwa na:
Mbunge wa Jimbo la Musoma Vijijini

**Prof. Dr.rer.nat. Sospeter M Muhongo**
Officier, Ordre des Palmes académiques
FGSAf, FAAS, MASSAf, FASI, FASSAf, FTAAS, FGIGE, FTWAS, HonRFCAGS, HonFGSA, HonFGS, CGeol, EurGeol

**Homepage/Tovuti:**
www.musomavijijini.or.tz

**Telephone/Simu:**
+255 754 400 800

**Date/Tarehe:**
30 Juni 2021